JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27

**Mhe. Mhandisi Hamad M. Y. Masauni (Mb.)**
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais
(Muungano na Mazingira)







DODOMA

APRILI, 2026

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27

**Mhe. Mhandisi Hamad M. Y. Masauni (Mb.)**
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais**
**(Muungano na Mazingira)**

# VIONGOZI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS



**Mhe. Balozi. Dkt. Emmanuel John Nchimbi**
**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



**Mhe. Mhandisi. Hamad Yussuf Masauni (Mb.)**
**Waziri wa Nchi (Muungano na Mazingira)**



**Mhe. Reuben Nhamanilo Kwagilwa (Mb.)**
**Naibu Waziri (Muungano na Mazingira)**



**Dkt. Richard Stanslaus Muyungi**
**Katibu Mkuu**



**Bw. Abdallah Hassan Mitawi**
**Naibu Katibu Mkuu (Muungano)**



**Balozi. Baraka Haran Luvanda**
**Naibu Katibu Mkuu (Mazingira)**

## A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/26 kufuatia mawasilisho yaliyotolewa na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Maji na Mazingira. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/27.

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai na afya njema ya kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/27.

### Salamu za Pongezi na Shukrani

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu**

**Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuchaguliwa tena kwa awamu ya pili kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hivyo kupata tena heshima na imani ya Watanzania ya kuweza kuliongoza taifa letu kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo. Heshima hii inatokana na uongozi wake mahiri na wa kipekee katika sehemu ya kwanza ya awamu ya sita ambapo wote tumeshuhudia mageuzi na maendeleo makubwa katika nchi yetu hususan, katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua tena katika awamu ya pili kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa Balozi **Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na kuendelea kutekeleza vyema jukumu lake la kikatiba la kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu pamoja

na kusimamia masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu nchini. Aidha, ninapenda kumshukuru kwa uongozi wake thabiti unaodhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri anayofanya katika kudumisha Muungano wetu, kusimamia hifadhi ya mazingira nchini na kuimarisha uchumi wa buluu.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kuchaguliwa kwake kwa mara ya pili kumetokana na uongozi wake thabiti aliouonesha katika muhula wake wa kwanza wa uongozi. Aidha, ninamshukuru kwa uongozi wake na maelekezo anayotupa katika kuimarisha mshikamano na ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa **Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali. Aidha, ninamshukuru kwa hotuba yake aliyoitoa bungeni

tarehe 1 Aprili, 2026 ambayo inatoa mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2026/27.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako Mheshimiwa **Mussa Azzan Zungu (Mb.),** kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninakushukuru kwa namna unavyoliongoza Bunge lako tukufu na ninaahidi kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kutoa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za nchi.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa **Daniel Baran Sillo (Mb.),** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya katika kumsaidia Spika wa Bunge kutekeleza majukumu yake.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza pia Mheshimiwa **Najma Murtaza Giga (Mb.),**

Mheshimiwa **Cecilia Daniel Paresso (Mb.),** na Mheshimiwa **Deodatus Philip Mwanyika (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninawapongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa **Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.),** na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Mheshimiwa **Jackson Gedion Kiswaga (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Kamati hizo. Aidha, ninawashukuru kwa dhati wajumbe wa kamati hizi mbili kwa kuendelea kunipatia ushirikiano madhubuti katika kutekeleza majukumu yangu ya usimamizi wa masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu. Vilevile, ninawapongeza waheshimiwa wenyeviti wa kamati mbalimbali za kudumu za Bunge waliochaguliwa kusimamia kamati hizo.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa, kuchaguliwa na kupewa dhamana kubwa na wananchi ya kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza

Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba uniruhusu niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa heshima na imani kubwa waliopata ya kuteuliwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninawashukuru kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kunipatia wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu nchini.

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa **Hamza Saidi Johari** kwa kuaminiwa na kuteuliwa tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, ninamshukuru kwa ushauri wake anaoendelea kutupatia wakati wa utekelezaji wa Majukumu yetu.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo mkunjufu ninapenda kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Festo John Dugange (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Naibu

Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kwa muda ambao nimefanya naye kazi alinishauri vyema na kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kumpongeza Mheshimiwa **Reuben Nhamanilo Kwagilwa (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Uchapakazi wake utakuwa nyenzo kubwa katika kuhakikisha Ofisi ya Makamu wa Rais inafikia malengo iliyojiwekea. Hakika kwa muda mfupi ambao nimeanza kufanya naye kazi ameonesha ushirikiano na weledi wa hali ya juu.



***Mhe. Reuben Nhamanilo Kwagilwa akiapishwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwenye hafla iliyofanyika Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma Aprili 08, 2026.***

## Salamu za Pole

**16.** ***Mheshimiwa Spika*****,** ninaomba kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa **William Vangimembe Lukuvi** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa **Jenista Joakim Mhagama** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa **Halima Idd Nassor** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi). Tunawaombea Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya salamu hizo na maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2025/26 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2026/27.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

### i. Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2025/26

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais kibajeti ina Mafungu mawili ambayo ni Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**Fungu 26:**

**19.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha mwaka 2025/26, jumla ya Shilingi **19,946,399,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, Shilingi **18,879,500,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **1,066,899,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara.

**Fungu 31:**

**20.** ***Mheshimiwa Spika****,* kwa upande wa Fungu 31, jumla ya Shilingi **47,917,792,000.00** ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **28,858,213,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **19,059,579,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha Shilingi **4,232,310,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Shilingi **6,675,287,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Shilingi **17,950,616,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo inajumuisha Shilingi **4,602,000,000.00** fedha za ndani na Shilingi **14,457,579,000.00** fedha za nje.

**ii. Fedha zilizopokelewa na kutumika hadi Machi, 2026**

**Fungu 26**

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya Shilingi **15,005,068,199.97** fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya

Fungu 26 sawa na asilimia 75.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **14,400,741,199.97** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 76.3 na Shilingi **604,327,000.00** ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 56.6 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya Shilingi **14,800,593,132.54** zilitumika sawa na asilimia 98.6 ya fedha zilizopokelewa.

**Fungu 31**

**22.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Fungu 31 lilipokea jumla ya **Shilingi 27,136,065,335.56** fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **3,378,708,300.00** ni mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais sawa na asilimia 79.8 ya bajeti iliyoidhinishwa, Shilingi **4,917,620,285.56** ni Mishahara ya Watumishi wa NEMC sawa na asilimia 73.7 ya bajeti iliyoidhinishwa, na Shilingi **18,839,736,750.00** ni Matumizi Mengineyo sawa na asilimia 83.8 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa, Shilingi **21,160,209,564.38** zilitumika, sawa na asilimia 78 ya fedha zilizopokelewa.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo, jumla ya Shilingi **17,576,799,447.45** zilipokelewa sawa na asilimia 92.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho, fedha za ndani ni Shilingi **10,798,369,447.45** na fedha za nje ni Shilingi **6,778,430,000.00.** Aidha, katika kipindi hicho, Shilingi **14,176,251,453.69** zilitumika ambapo Shilingi **9,076,833,816.69** ni fedha za ndani sawa na asilimia 84 ya fedha zilizopokelewa na Shilingi **5,099,417,637.00** ni fedha za nje sawa na asilimia 75.2 ya fedha zilizopokelewa.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 47(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu; Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sera ya Taifa ya uchumi wa Buluu ya mwaka 2024; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na marekebisho yake na kanuni zake; na Miongozo na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Viongozi Wakuu.

## C. KAZI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026

### 1) MASUALA YA MUUNGANO

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mwaka huu 2026 Muungano wetu unatimiza miaka 62 tangu kuasisiwa kwake. Wote mtakubaliana nami kuwa tuna jukumu la kuulinda, kuudumisha na kuimarisha Muungano wetu. Hivyo, hatuna budi kukumbuka tukio hili muhimu na kuendeleza mafanikio makubwa yaliyopatikana kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, ni muhimu kuendeleza amani, umoja, ushirikiano na kuheshimiana baina ya pande zote mbili za Muungano. Serikali itaendelea kuulinda, kuudumisha na kuimarisha Muungano wetu adhimu na adimu.

**26.** ***Mheshimiwa Spika*,** mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika mambo yasiyo ya Muungano. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

a) **Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano**

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Ofisi imefanya mapitio na kuchapisha Mwongozo mpya wa Vikao vya Kamati ya Pamoja kati ya SJMT na SMZ, Toleo la 2025. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine umeainisha jukumu jingine la vikao kuwa ni kujadili masuala mengine yenye maslahi mapana ya pande mbili ikiwemo fursa zilizopo pande mbili za Muungano na si kujadili hoja za Muungano pekee, kwa kuwa kila upande zipo fursa zinazoweza kutumika kwa pamoja au kwa kushirikiana na hivyo kuwa na uelewa wa pamoja wa fursa za pande mbili za Muungano na kuzitolea maamuzi.

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwaka 2025/26 jumla ya Hoja 22 kati ya Hoja 25 zimepatiwa ufumbuzi na hoja tatu zilizobakia zinaendelea kufanyiwa kazi. Hoja hizo ni pamoja na hoja inayohusu masuala ya kifedha (mgawanyo wa mapato yatokanayo na Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki,

Faida ya Benki Kuu na Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha); Usajili wa vyombo vya moto; na Uingizaji wa Sukari inayozalishwa Zanzibar katika soko la Tanzania Bara. Serikali zote mbili zina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba hoja zote zilizobakia zinapatiwa ufumbuzi.

### *b)* Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa tunaondosha ombwe la changamoto ya uelewa kwa Umma kuhusu elimu ya Muungano hususan kwa vijana, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Mpango Kabambe wa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano. Mpango huo unahusisha shughuli mbalimbali ikiwemo semina, makongamano, muungano caravan, mashindano ya michezo, mashindano ya insha na programu za redio na televisheni. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika kupitia Mpango huo ni pamoja na utolewaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilitoa semina kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari zilizofanyika Zanzibar

tarehe 19 Desemba, 2025 na Dar es Salaam tarehe 23 Desemba, 2025.



***Wahariri wa Vyombo vya Habari mbalimbali wakishiriki Semina ya kujenga uelewa kuhusu Muungano iliyofanyika jijini Dar es Salaam Desemba 23, 2025.***



***Wahariri wa Vyombo vya Habarl mbalimbali wakishiriki Semina ya kujenga uelewa kuhusu Muungano iliyofanyika Zanzibar Desemba 19, 2025.***

31. ***Mheshimiwa Spika**,* Aidha, Ofisi ilitoa Semina kuhusu masuala ya Muungano kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ukumbi wa Pius - Msekwa Jijini Dodoma tarehe 11 Februari, 2026 na tarehe 27 Februari, 2026 kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, katika Ukumbi wa Mikutano wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.



***Sehemu ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakishiriki Semina ya kujenga uelewa kuhusu Muungano iliyofanyika jijini Dodoma Februari 11, 2026.***



*Sehemu ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakishiriki Semina kuhusu Muungano iliyofanyika Unguja, Zanzibar, Februari 27,2026*

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, Vilevile Ofisi iliandaa na kuratibu Makongamano kuhusu masuala ya Muungano kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya juu wa Vyuo vilivyopo Zanzibar lililofanyika tarehe 19 Februari, 2026 katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.



*Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Zanzibar wakishiriki Kongamano kuhusu Muungano lililofanyika katika Mkoa wa Kusini, Unguja Februari 19, 2026.*

**33.** ***Mheshimiwa Spika****,* tarehe 6 Aprili, 2026 Ofisi kwa kushirikiana na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ilifanya Kongamano la Kumuenzi Hayati Sheikh Abeid Amani Karume lililobeba maudhui ya **Mwanamajumui wa Afrika, Mwasisi wa Muungano na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar**. Kongamano hili lilifanyika Dar es Salaam katika Ukumbi wa Karimjee, Ukumbi ambao unabeba historia muhimu ya Taifa la Tanzania kwani matukio mengi muhimu ya kuanzishwa kwa Muungano yalifanyika katika Ukumbi wa Karimjee ikiwemo kuapishwa kwa Sheikh Abeid Amani Karume kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.




***Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni akiwa pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Mhe. Hamza Hassan Juma wakiwasili katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kushiriki Kongamano la Kumbukumbu ya Miaka 54 ya Kifo cha Sheikh Abeid Amani Karume lililofanyika Aprili 6, 2026.***

**34.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika kuendeleza jitihada za kutoa elimu kwa umma, Ofisi ilifungua Akaunti mahsusi za mitandao ya kijamii kwa lengo la kuwafikia vijana na kutoa taarifa sahihi kuhusu Muungano. Akaunti hizo ni za *Instagram, Facebook, Youtube, X,* na *Chatbox* zijulikanazo kwa jina la **miminamuungano** ambazo zinasaidia kuondoa upotoshaji unaofanywa na wasioutakia mema Muungano kupitia mitandao ya kijamii. Katika kipindi cha Januari hadi Februari, 2026 watu waliofikiwa ni

1,800,000. Aidha, jumla ya machapisho 585 yalichapishwa na kusambazwa kupitia mitandao hiyo. Naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa wabunge wote na wananchi kwa ujumla kutembelea akaunti hizi za mitandao ya kijamii ya **#miminamuungano** ili kupata taarifa sahihi kuhusu muungano na kusaidia kuelimisha jamii.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeandaa na kuchapisha vitini vya maswali na majibu kuhusu Muungano kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya Muungano hususan maswali yanayoulizwa mara kwa mara.




**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kukusanya kumbukumbu na nyaraka za Muungano kwa ajili ya uanzishwaji wa Vituo vya Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano ikiwemo kumbukumbu, nyaraka, vifaa, video na tasnifu (tafiti) kutoka Taasisi kadhaa.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutumia mbinu mbalimbali za kuwaelimisha wananchi kuhusu Muungano ikiwemo kupitia makala mjongeo kwenye vyombo vya usafiri kama vile treni ya mwendokasi (SGR) na boti ziendazo kasi (AZAM Marine), ambapo maudhui mbalimbali kuhusu Muungano hurushwa ikiwemo hatua za Muungano, Faida za Muungano na Viongozi waliohudumu kwenye nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1964 hadi sasa.




***Muonekano wa makala mjongeo kwenye treni ya mwendokasi inayotoa elimu ya Muungano kwa wananchi wanaosafiri.***

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 26 Agosti, 2025**,** Ofisi ilitoa mafunzo kwa Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara zote za SJMT ambapo moja ya wasilisho lilihusu Majukumu ya Wakurugenzi wa Sera na Mipango katika kulinda na kuimarisha Muungano na umuhimu wa kuzingatia vipaumbele vinavyohusu Muungano katika mipango na Bajeti za Sekta zao.



***Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais Prof. Peter Msoffe (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Wakurugenzi wa Sera na Mipango mara baada ya kufungua kikao cha Wakurugenzi wa Sera na Mipango kutoka wizara za kisekta na taasisi kilichofanyika Dodoma Septemba 2, 2025.***

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilishiriki na kutoa elimu kuhusu Muungano katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane), Siku ya kumbukumbu ya Mapinduzi, Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) na Siku ya Mazingira Duniani.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliendelea kurusha vipindi katika Vyombo vya Habari vya TBC na ZBC

Redio na TV kupitia kipindi maalum cha '*Hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania'*.

**41.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika kuhakikisha kwamba Muungano unaimarishwa kupitia michezo, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar na Wizara zenye dhamana ya michezo kutoka pande zote mbili za Muungano pamoja na Mashirikisho ya Vyama vya Michezo Tanzania (TFF na ZFF) tumefanikiwa kurejesha mashindano ya Muungano kwa Mpira wa Miguu yaliyokuwa yamesimama kwa miaka 20. Kwa mwaka huu mashindano haya yanatarajiwa kufanyika tarehe 21 hadi 29 Aprili, 2026 na yatahusisha timu nane (Simba, Yanga, Azam, Singida Black Stars, Mlandege FC, Mwembe Makumbi City, Mafunzo SC na KVZ FC).

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mpira wa Pete (Netiboli), kwa mara ya kwanza Timu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ilishiriki mashindano ya ligi ya Netiboli ya Muungano yaliyofanyika Zanzibar katika Viwanja vya Netiboli vya *New Amaan Complex* kuanzia tarehe 15 hadi 24 Januari, 2026. Lengo la

mashindano hayo ni kudumisha Muungano, kujenga umoja na mshikamano, kuleta burudani pamoja na kuboresha afya. Aidha, mashindano ya Mieleka ya kombe la Muungano yameanzishwa kwa mara ya kwanza mwaka huu 2025/26. Ofisi ilitumia mashindano hayo kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano.



***Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na viongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na wachezaji wa Timu ya Netiboli ya Ofisi hiyo baada ya kukabidhiwa Kombe na vyeti ambavyo imepata katika mashindano maalum ya Ligi ya Muungano iliyofanyika Zanzibar Januari 15 hadi 24, 2026 wakati wa Hafla ya kuwafuturisha wachezaji hao nyumbani kwake Dodoma Machi 11, 2026.***

## c) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu gawio kwa SMZ ambapo hadi kufikia Machi, 2026

jumla ya shilingi bilioni **48.5** zilipelekwa Zanzibar. Fedha hizo zinajumuisha gawio la *PAYE* kwa watumishi wa Zanzibar wanaofanya kazi Tanzania Bara - shilingi bilioni 14; Misaada Nafuu ya Kibajeti (GBS) - shilingi bilioni 21; na gawio la faida ya Benki Kuu - shilingi bilioni 13.5.

### d) Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Zanzibar

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea na usimamizi na uratibu wa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa wabunge wa majimbo 50 ya Zanzibar kwa mujibu wa kifungu 4(2) cha Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Sura 96. Aidha, katika kujenga uelewa mpana juu ya usimamizi na matumizi ya fedha za Mfuko wa jimbo pamoja na kupokea maoni ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo, tarehe 26 Februari, 2026 Ofisi iliandaa na kutoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wakurugenzi wa Halmashauri, Manispaa na Mabaraza ya Miji ya Zanzibar ambao ndio wasimamizi wa miradi inayotekelezwa na fedha hizo.




***Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla (katikati) pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Mhe. Hamza Hassan Juma katika picha ya pamoja na baadhi ya Wabunge kutoka Zanzibar walioshiriki Semina Kuhusu Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, iliyofanyika Zanzibar Februari 26, 2026.***

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** *katika mwaka 2025/26* Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 50 ya Zanzibar, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 jumla ya shilingi bilioni **2.034** zimepelekwa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika sekta ya elimu, afya, maji, barabara na shughuli za kijamii.

**e) Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu

utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kama yalivyoainishwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) ambapo Wizara, Idara na Taasisi za Muungano zinatekeleza majukumu hayo.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Muungano na kuhakikisha kuwa Taasisi hizo zinatoa huduma stahiki kwa wananchi wa pande mbili za Muungano.

### f) Miradi na Programu za Maendeleo zinazotekelezwa pande mbili za Muungano

**48.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2025/26, Serikali imeendelea kuwezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo. Miradi na programu hizo zimefanikiwa kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuboresha ustawi wa jamii.

**49.** ***Mheshimiwa Spika****,* miradi na programu hizo ni pamoja na: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii chini ya TASAF; Mfuko wa Elimu chini ya Mamlaka ya Elimu

Tanzania (TEA); Mradi wa kusafirisha Umeme kupitia Baharini wa Msongo wa Kilovoti 220 kwenda Zanzibar, Kilovoti 132 kwenda Pemba, na Kilovoti 33 kwenda Mafia kupitia Wizara ya Nishati ambao upo katika hatua za utekelezaji.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, *TEA* imeweza kunufaisha wanufaika 8,180 kwa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar, wanufaika 8,720. Aidha, kwa upande wa Zanzibar TEA imefanikiwa kuanza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Amali katika eneo la Kangagani – Pemba na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Amali katika eneo la Kizimkazi, Unguja.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi mingine inayotekelezwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) Tanzania Bara na Zanzibar ni pamoja na: Mfumo wa mawasiliano ya redio kati ya marubani na vituo vya kuongozea ndege; Mradi unaotoa taarifa muhimu kwa marubani; na Mradi wa kwa ajili ya kubadilishana taarifa za anga kwa njia ya kidijitali baina ya Taasisi mbalimbali.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais

imeendeleza ushirikiano na Zanzibar katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya Tabianchi ambapo miradi ya mazingira imekuwa ikitekelezwa pande zote mbili za Muungano. Miradi hiyo ni pamoja na Miradi ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kutokana na kuongezeka kwa kina cha Bahari ya Hindi - Sipwese Pemba; na mradi wa kuimarisha jamii na mifumo ikolojia katika kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa misitu ya miombo Tanzania Bara na maeneo kame ya Zanzibar. Aidha, pande mbili zinaendelea kutafuta kwa pamoja fedha za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kutoka katika mifuko ya kimataifa kwa lengo la kufanikisha miradi ya mazingira na kufikiwa kwa malengo ya Nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuleta mchango katika maendeleo ya Taifa.

**g) Kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya SJMT na SMZ**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya SJMT na SMZ ambapo jumla ya vikao kumi na

tano (15) vya Ushirikiano na Wizara za Kisekta za (SJMT) na (SMZ) vilifanyika kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa Sera, Sheria na utaalamu katika maeneo mbalimbali. Sekta zilizofanya vikao ni: Elimu; Mazingira; Uchumi wa Buluu; Uratibu wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano; Sera na Tafiti; Uchunguzi; Mifugo na Uvuvi; Maji; Fedha; Mambo ya Ndani; Kilimo; Ujenzi; Michezo; Teknolojia ya Habari; na Biashara.



***Aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Festo Dugange pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Mhe. Hamza Hassan Juma wakiwa na watendaji waandamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar mara baada ya kikao cha Ushirikiano kilichofanyika Zanzibar Februari 16, 2026.***

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilifanya ziara maalum ya kutembelea Viongozi Wastaafu wa SJMT na SMZ kwa lengo kupata maelekezo, maoni na uzoefu wao katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais hususan katika kulinda na kudumisha Muungano.



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, alipomtembelea Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mstaafu wa Zanzibar katika makazi yake Unguja, Zanzibar, Januari 03, 2026.***



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akizungumza na Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume alipomtembelea katika makazi yake Unguja, Zanzibar Januari 03, 2026.***



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, alipomtembelea Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, katika makazi yake Masaki Jijini Dar es Salaam, Januari 02, 2026.***

### 2) HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kama unavyofahamu***,*** tarehe 17 Julai, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 ambayo mojawapo ya nguzo zake tatu inahusu Uhifadhi wa Mazingira na ustahimilivu dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, Ibara ya 3.1.7 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030 imeweka masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kama mojawapo ya masuala muhimu yatakayozingatiwa katika kipindi husika.

**56.** ***Mheshimiwa Spika****,* Hii ni zaidi ya uthibitisho kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu mpendwa imetoa kipaumbele kwa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kama msingi wa ukuaji wa uchumi na ustawi wa watanzania.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la

kuhakikisha kuwa watanzania wote wanaendelea kuishi katika mazingira bora na salama. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira, kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kama nyenzo mojawapo ya kuimarisha uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kuhamasisha upandaji miti, na uwekezaji katika biashara ya Kaboni. Hata hivyo, jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili, uhifadhi wa mazingira umeendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: Uharibifu wa ardhi; Ukataji ovyo wa miti na uharibifu wa misitu unaochangiwa na utegemezi wa matumizi ya nishati ya kuni na mkaa; Kilimo cha kuhamahama; Uchafuzi wa mazingira; Upotevu wa makazi ya wanyamapori na bioanuai; Uharibifu wa vyanzo vya maji, mifumo ikolojia ya ukanda wa pwani na bahari; Kuenea kwa viumbe vamizi; na Athari za mabadiliko ya tabianchi. Changomoto hizi zinachangiwa zaidi na uwepo wa shughuli za

kibinadamu zisizo endelevu zinazofanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo, Mikakati, Miradi ya hifadhi ya mazingira, na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Hifadhi ya Mazingira na mabadiliko ya tabianchi ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama. Kwa mwaka 2025/26, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza yafuatayo:

a) **Kuratibu Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 ikiwa ni pamoja na:

i. **Kuratibu Masuala ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika Wizara za kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za**

### Serikali za Mitaa

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kuwatumia Maafisa Viungo walioteuliwa ili kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira kwenye Wizara, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizofanyika ni pamoja na kufanya:- Vikao vya kimkakati na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Dodoma kuhusu hatua za kuimarisha usafi wa mazingira na udhibiti wa taka kwa kuzingatia dhana ya uchumi rejeshi (circular economy); Wataalamu wa Mazingira (48) kutoka Sekretarieti za Mikoa na Maafisa (50) kutoka Wizara za Kisekta walijengewa uwezo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka (2025-2030), na Mpango wa Taifa wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi (2025-2030).

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi pia iliratibu kikao-kazi na kuwajengea uwezo Wakurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara za Kisekta kuhusu ujumuishaji wa masuala ya mazingira yaliyoainishwa kwenye Dira

2050 katika mipango na bajeti ya Wizara na Taasisi za Umma; Vilevile, wajumbe (25) wa Kamati ya Kitaifa ya ushauri kuhusu Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi walijengewa uwezo kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa Sheria. Sambamba na hilo, katika kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Ofisi iliratibu Kikao cha Mashirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichofanyika Zanzibar tarehe 16 - 17 Februari, 2026 ambapo pamoja na masuala mengine mikakati ya ushirikiano iliyoafikiwa ni pamoja na; kuimarisha biashara ya kaboni; kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; kujenga uwezo wa kitaalamu katika hifadhi na usimamizi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; Kuanzishwa kwa mashirikiano rasmi baina ya Mamlaka ya Mazingira Zanzibar (ZEMA) na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ikiwemo ukamilishwaji na utiwaji wa saini wa Hati ya

Mashirikiano baina ya Taasisi hizo.



***Aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Festo Dugange (mbele katikati) akiwa na viongozi na wataalamu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) mara baada ya kikao cha ushirikiano kilichofanyika Februari 17, 2026, Zanzibar.***

**b) Kuratibu Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

**i. Kanuni na Mikakati ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imefanya mapitio ya Marekebisho ya Kanuni za Ada na Tozo kupitia Tangazo la Serikali Na. 494/2025. Aidha, kabla ya mwaka huu wa fedha kukamilika, Ofisi ya Makamu wa Rais itakamilisha Kanuni za Udhibiti wa Kemikali zinazodumu kwenye Mazingira kwa Muda Mrefu pamoja na Kanuni za

Katazo la Matumizi ya Kuni na Mkaa.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26 Ofisi imeandaa Mipango na Mikakati mbalimbali ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Mipango na mikakati hiyo ni pamoja na: Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame (National Action Program to Combat Desertification, 2025-2030), Taarifa ya Tatu ya Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Nationally Determined Contribution - NDC 3.0); Mpango wa Taifa wa kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi (National Adaptation Plan, NAP (2025 – 2035); na Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Uhifadhi wa Bioanuai (National Biodiversity Strategy and Action Plan, NBSAP, 2025 - 2030).

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2025-2030) umejumuisha mikakati na hatua mahsusi za kuimarisha usimamizi endelevu wa ardhi, kuhifadhi na kurejesha uoto wa asili, kuboresha ustahimilivu wa jamii dhidi ya athari za ukame, pamoja na kuimarisha uratibu wa taasisi, ufuatiliaji na tathmini

ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na kuenea kwa hali ya jangwa nchini. Mpango huu utatekelezwa zaidi kwenye maeneo kame na utachangia katika kupunguza kuenea kwa hali ya jangwa nchini.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Taifa wa kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi (2025 – 2035) umeainisha jitihada mbalimbali zinazotakiwa kuchukuliwa ili kuimarisha uhimilivu wa jamii, mifumo ikolojia na sekta za ukuaji wa uchumi dhidi ya athari za mabadiliko ya Tabianchi. Mpango huu umebainisha sekta tisa (9) za kipaumbele zinazoathiriwa zaidi na mabadiliko ya Tabianchi na kuweka mikakati mahsusi ya kukabiliana na changamoto hiyo. Sekta hizo ni Kilimo, Maji, Uvuvi, Mifugo, Wanyamapori, Miundombinu, Afya, Utalii, na Rasilimali za Ukanda wa Pwani na Bahari.

**67.** ***Mheshimiwa Spika*****,** sambamba na hilo Ofisi imeratibu maandalizi ya Taarifa ya Mchango wa Taifa wa tatu wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Nationally Determined Contribution - NDC 3.0). Aidha, taarifa hiyo imezingatia vipaumbele, maslahi na mahitaji ya nchi yetu katika maeneo yanayohusu

ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na kupunguza uzalishaji wa gesijoto. Nyenzo hizi zilizoandaliwa zinatoa mwongozo wa kitaifa na kubainisha majukumu mahsusi ya wadau katika juhudi za Taifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**68.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuimarisha uhifadhi wa bioanuai na mifumo-ikolojia, Ofisi imeratibu maandalizi ya Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Uhifadhi wa Bioanuai (2025 - 2030). Mkakati huu una malengo manne (4) yanayoendana na Mpango wa kidunia wa kuhifadhi bioanuai. Malengo hayo yanahusu masuala ya kudhibiti upotevu wa Bioanuai, kuongeza upatikanaji wa huduma za kiikolojia kwa watu na viumbe hai, upatikanaji wa fedha za kuwezesha hifadhi ya bioanuai na ushirikishwaji wa makundi mbalimbali ya kijamii ikiwemo wanawake na vijana. Mkakati huu wa kitaifa, umezingatia masuala ya hifadhi ya mazingira yaliyopo katika Dira 2050 na utatumika katika utafutaji wa fedha za ndani na nje za kuhifadhi bioanuai.

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba nitumie Bunge lako tukufu kuendelea kuhimiza wadau ndani na nje ya

Serikali kuhakikisha kuwa wanatenga bajeti kuwezesha utekelezaji wa afua mahsusi zilizobainishwa katika mipango na mikakati hiyo ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya Nguzo ya Tatu ya Dira 2050 ya hifadhi ya Mazingira na ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi.

### ii. Utoaji wa Vibali vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK)

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imetoa vibali sita (06) vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK) kwa ajili ya:- Programu ya Ufugaji wa Samaki kwa njia ya Vizimba katika Mikoa ya kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Mwanza, Simiyu, Mara na Geita); Programu ya Mfumo Ikolojia wa Mikumi; Mpango kabambe wa Uendelezaji wa eneo la Kasabi katika Halmshauri ya Kibaha Mkoa wa Pwani; Mradi wa Uboreshaji wa Bonde la Msimbazi; Kongani ya Viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo hususan zao la Korosho, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, Mkoa wa Mtwara; na Eneo la Maalum la Kiuchumi la Buzwagi, katika Halmashauri ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga.

### c) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032)

.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango huu, Ofisi imeendelea kuratibu upatikanaji wa fedha kupitia mifuko ya kimataifa ya Mazingira na kukabiliana na Mabadiliko ya tabianchi ili kutekeleza miradi mbalimbali. Aidha, Miradi mitano imeidhinishiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Miradi hiyo ni: Mradi wa kuboresha mifumo ya chakula Nyanda za juu kusini mwa Tanzania Bara na Zanzibar. Mradi huu utatekelezwa katika mikoa ya Njombe (Wanging'ombe), Mbeya (Mbarali na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya), Iringa (Makete), Kaskazini Unguja (Kaskazini B), Kaskazini Pemba (Wete) na Kusini Pemba (Chakechake). Mradi wa Usimamizi Shirikishi na Hifadhi endelevu ya Ikolojia ya Bonde la Mto Wami – Ruvu; Mradi huu unatekelezwa katika mikoa ya Dodoma (Bahi, Chamwino, Dodoma Jiji na Kongwa), Morogoro (Mvomero), Pwani (Kibaha) na Dar es Salaam (Ilala). Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uimarishaji wa Ustahimilivu wa Jamii katika

maeneo kame na vituo vya uhamaji wa Mifugo nchini Tanzania. Mradi huu utatekelezwa katika mikoa ya Simiyu (Meatu), Manyara (Simanjiro), Shinyanga (Kishapu), Arusha (Monduli), Tabora (Igunga), Dodoma (Chemba) na Singida (Ikungi).

**72.** ***Mheshimiwa Spika***, Miradi mingine ni mradi wa Kuendeleza Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia vijijini. Mradi huu utatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya nane (8) ambazo ni: Bunda, Serengeti, Tarime, Ngorongoro, Karatu, Meatu, Busega na Mbulu; na Mradi wa Urejeshwaji na Uhifadhi Endelevu wa Mfumo wa Ikolojia wa Bonde Oevu la Malagarasi–Moyowosi kupitia Mbinu Jumuishi za hifadhi ya bioanuai. Mradi huu utatekelezwa katika Mikoa ya Kigoma (Kasulu na Uvinza), na Tabora (Kaliua na Urambo). Miradi hii kwa ujumla ina thamani ya kiasi shilingi bilioni 102.3.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi hii inalenga katika kukabiliana na visababishi vya uharibifu wa mazingira ambavyo vinatokana na shughuli za kibinadamu zisizoendelevu pamoja na kujenga uwezo wa jamii katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Shughuli za kimkakati zitakazotekelezwa zitahusisha: Masuala ya urejeshaji wa mifumo ikolojia ya misitu na vyanzo vya maji; Shughuli za ufugaji wenye tija na kilimo endelevu kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi; Kuwezesha upatikanaji wa maji katika ngazi ya kaya; na Shughuli mbadala za kiuchumi ambazo ni rafiki kwa mazingira.

**74.** ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kupitia Bunge lako Tukufu niendelee kuhimiza Wizara, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wanajumuisha katika mipango na bajeti masuala mahsusi ya mazingira yanayohusu sekta zao yaliyobainishwa katika Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

### d) Nishati Safi ya Kupikia

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024- 2034) kwa kuhamasisha matumizi ya Nishati safi ya kupikia kwa taasisi za umma na binafsi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku, ambapo hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya taasisi

1,350 zimeanza matumizi ya nishati safi ya kupikia zikiwemo Shule za Msingi na Sekondari; Vyuo vya Kati na Ualimu; Magereza; Hospitali; Jeshi la Kujenga Taifa; Hoteli; Migahawa; Mama na Baba lishe.



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (mwenye skafu) akimsikiliza Mkuu wa Wilaya ya Geita Mhe. Hashim Komba wakati alipotembelea Shule ya Sekondari ya Wasichana Geita kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya kutumia nishati safi kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100.***

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati iliendesha mafunzo kwa maafisa dawati 30 wa nishati safi ya kupikia kutoka katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es salaam, Lindi na Mtwara kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa ufuatiliaji na uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034.

77. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kutumia Bunge lako Tukufu kuhimiza taasisi zilizobaki zinazolisha watu zaidi ya 100 kuhakikisha kuwa zinatumia nishati safi ya kupikia kwa mujibu wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa lililotolewa na Serikali Januari, 2024. Vilevile, natoa rai kwa sekta binafsi hususan makampuni yanayouza majiko na teknolojia za nishati safi kuendelea kuweka mazingira wezeshi na nafuu ili kuchochea matumizi ya nishati safi nchini.

### e) Elimu kwa Umma Kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

78. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia vyombo vya habari, makongamano, semina, warsha na maonesho ya kitaifa na kimataifa. Aidha, kupitia kipindi maalumu kiitwacho **"Mazingira Yetu na Tanzania Ijayo"** jumla ya vipindi tisa (9) vya runinga, 14 vya redio vilirushwa na habari 655 za kuelimisha umma zilitolewa kupitia magazeti. Vipindi hivyo vilihusu, Matumizi ya nishati Safi ya kupikia, Udhibiti

wa Taka Ngumu, Fursa za Uwekezaji katika Sekta ya Mazingira ikiwemo Biashara ya Kaboni, Kampeni ya Upandaji Miti, Udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la Ozoni, na Uhamasishaji wa Usafi wa Mazingira.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, elimu kwa umma imetolewa kupitia maadhimisho ya kitaifa, kikanda na kimataifa yanayohusu mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Maadhimisho hayo ni pamoja na: Siku ya Ardhi Oevu, tarehe 2 Februari; Siku ya Mazingira Afrika, tarehe 3 Machi; Siku ya Misitu Duniani, tarehe 21 Machi; Siku ya Maji Duniani, tarehe 22 Machi; na Kuenea kwa Jangwa na Ukame, tarehe 17 Juni; na Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni tarehe 16 Septemba.

### f) Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji miti milioni 1.5 katika kila Halmashauri nchini ambapo hadi kufikia Machi, 2026 takriban asilimia 76 ya miti iliyopandwa imestawi.



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akimwagilia mti aina ya mwembe aliopanda wakati alipowasili katika Ukumbi wa Chimwaga jijini Dodoma, kwa ajili ya ufunguzi wa Kongamano la Vijana katika Kumbukizi ya Miaka 104 ya Kuzaliwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Aprili 11, 2026.***

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kampeni hii, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Jiji la Dodoma imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kujihusisha na suala la kukijanisha Jiji la Dodoma. Hadi Machi, 2026 jumla ya miti 960,210 imepandwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji na iliyostawi ni miti 787,372 sawa na asilimia 82. Aidha, Ofisi itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kuwa zoezi la upandaji miti katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma linakuwa endelevu kwa ajili ya kupambana

na ukame na kuboresha mandhari ya Jiji. Aidha, katika kuimarisha uhifadhi wa mifumo ikolojia ya milima na vilima katika Jiji la Dodoma, Ofisi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma imepanga kudhibiti uharibifu wa maeneo hayo kutokana na shughuli za kibinadamu zisizo rafiki kwa mazingira pamoja na kuweka utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi katika kuwekeza katika shughuli za kiuchumi ambazo zinaendana na misingi ya uhifadhi wa mazingira.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhimiza na kuhamasisha upandaji na utunzaji wa miti nchini hususan kwa kuamua kutumia kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa kwake tarehe 27 Januari kila mwaka kupitia kampeni ya "**27 ya Kijani, Mti wa Mama,**" kuwa jukwaa la uhamasishaji wa upandaji miti.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile naomba nitoe pongezi kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kwa kutoa mchango wake mkubwa katika uhamasishaji wa

Kampeni ya ‘27 ya Kijani, Mti wa Mama’ pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na wadau wengine.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwahamasisha wananchi, taasisi na sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kiraia na wadau wengine kufuata nyayo za Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kupanda miti na kuitunza hasa katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha.

### g) Ushiriki wa Nchi Katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

**85.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi iliratibu na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kama ifuatavyo:-

**i) Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi**

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Belem, Brazil tarehe 10 hadi 21 Novemba, 2025. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa **Balozi Dkt. John Stephen Simbachawene**, Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Brazil akimwakilisha Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliongoza Kundi la Majadiliano la Wataalamu wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Dkt. Richard Stanslaus Muyungi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kundi hilo.



***Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Brazil Mhe. Balozi Dkt. John Stephen Simbachawene (kushoto) akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Belem, Brazil Novemba 10 hadi 21, 2025.***

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baadhi ya maazimio yaliyoafikiwa katika Mkutano huo ni pamoja na kupitishwa kwa vigezo vitakavyotumika kufanya tathmini ya nchi zitakazonufaika na fedha za utekelezaji wa miradi kupitia ufadhili wa Mfuko wa Kushughulikia Uharibifu na Hasara (The Fund for Responding to Loss and Damage) zitokanazo na athari za mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, iliazimiwa kuwa nchi nufaika zinaweza kupata ruzuku kati ya Dola za Marekani Milioni 5 hadi 20 kwa kila dirisha

litakalokuwa linatangazwa na mfuko husika. Ili kupata ruzuku hizo, Tanzania inakamilisha andiko la mradi chini ya Mfuko husika.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika majadiliano kuhusu malengo ya Dunia ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi, nchi wanachama zilikubaliana kupitishwa kwa viashiria 59 vitakavyotumika kupima utekelezaji wa shughuli za uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Uamuzi huu utasaidia kuimarisha ustahimilivu na kupunguza hatari zitokanazo na athari za mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuchangia katika utekelezaji wa Makubaliano ya Paris. Maazimio mengine yaliyofikiwa ni pamoja na: Nchi zinazoendelea kukataa maombi ya nchi zilizoendelea ya kutokutumia makaa ya mawe na gesi asilia ili kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na Nchi wanachama kuanza kutekeleza programu ya ubunifu wa teknolojia na uhaulishaji wake kwa nchi zinazoendelea.



***Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Richard Muyungi (kushoto) wakati huo akiwa Mwenyekiti wa Kundi la Majadiliano la Afrika (AGN,) akiwasilisha taarifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Nchi 54 kwenye Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Belem, Brazil Novemba 10 hadi 21, 2025.***

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano huu umeleta tija kwa Taifa ambapo Tanzania iliweza kupata ahadi ya fedha kutoka katika Mifuko, Washirika wa maendeleo na Wadau mbalimbali wa Mkataba huo zinazotokana na mikutano ya uwili baina ya Tanzania na mashirika ya kimataifa. Jumla ya Dola za Marekani Milioni 868.42 na Euro 500,000 ziliahidiwa kutolewa kwa Tanzania kwa ajili ya program na Miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi, Nishati safi ya kupikia, usimamizi wa Taka na uhifadhi wa bioanuai. Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya kiasi cha shilingi Bilioni 24 kimepatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwenye

vyanzo vya maji katika Bonde la Wami-Ruvu katika mto Mkondoa.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** mikutano mingine iliyofanyika chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi inajumuisha: Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika tarehe 8 – 10 Septemba, 2025 Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mkutano huo ulipitisha Azimio la Viongozi wa Afrika kuhusu mabadiliko ya tabianchi na wito wa kuchukua hatua kupambana na mabadiliko ya tabianchi; na Mkutano wa Matumizi ya Akili Unde katika Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi ukiwa na lengo la kuongeza ufanisi wa matumizi ya teknolojia ya Akili Unde katika sekta za Kilimo, Misitu, Maji, Umwagiliaji na udhibiti wa majanga ya asili uliofanyika Dar es Salaam tarehe 8-9 Oktoba 2025.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine makubwa yaliyopatikana katika medani ya kimataifa katika masuala ya mazingira ni pamoja na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitishwa rasmi

kuwa mjumbe wa kudumu wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya Umoja wa Afrika kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, Umoja wa Afrika ulipitisha Azimio la kumtambua rasmi **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kuwa kinara wa uhamasishaji wa masuala ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na: Jiji la Dar es Salaam kuwa mwenyeji wa Ofisi ya Kikanda ya Kujenga Uwezo wa nchi zinazoendelea katika kukabiliana na Upotevu na Hasara zitokanazo na athari za Mabadiliko ya Tabianchi (Regional Office for Santiago Network on Loss and Damage); na nchi yetu kuwa mwenyeji wa Kituo Mahiri cha Afrika cha Kujenga uwezo wa Vijana kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

### ii) Mkutano wa 27 wa Kamati ya kitaalamu chini ya Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 27 wa Kamati ya Ushauri wa Kitaalamu wa

Mkataba wa hifadhi ya Bioanuai uliofanyika tarehe 20 hadi 30 Oktoba, 2025 Panama. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Dunia wa Kuhifadhi Bioanuai.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano huo ni pamoja na nchi wanachama: Kuendeleza sera zinazoimarisha kilimo rafiki kwa mazingira na kupunguza uharibifu wa makazi asilia; Kuanzisha programu za kitaifa za kutathmini athari za kilimo kwa bioanuai; Kuwezesha mataifa kupata teknolojia, fedha na ujuzi wa utafiti kuhusu kilimo endelevu; Kuimarisha udhibiti wa viumbe vamizi katika mipaka; na kuwezesha nchi kutengeneza mifumo ya tahadhari ya mapema.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** manufaa yaliyopatikana kupitia ushiriki katika Mkutano huo ni pamoja na kujengewa uwezo kwa wataalam kuhusu tathmini ya hali ya uhifadhi wa bioanuai, rasilimali fedha zinazohitajika kuhifadhi bioanuai nchini na tathmini zingine ambazo ziliwezesha uandaaji wa Mkakati na Mpango kazi wa Taifa wa Uhifadhi wa Bioanuai (2025-

2030). Aidha, katika ushiriki wa mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata kiasi cha fedha jumla ya shilingi **931,791,960.00** kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuimarisha Uhifadhi na Usimamizi wa bioanuai nchini.

**iii) Mkutano wa 15 wa nchi wanachama wa Mkataba wa RAMSAR kuhusu uhifadhi wa ardhi oevu**

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa 15 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Ramsar kuhusu ardhi oevu uliofanyika Victoria Falls, Zimbabwe, tarehe 23 hadi 31 Julai, 2025. Maazimio ya Mkutano ni pamoja na: Kuongeza bajeti katika usimamizi na utekelezaji wa Sera, mipango, kanuni na mikakati ya kusimamia maeneo ya ardhi oevu; Nchi wanachama kutengeneza mfumo kwa kutafuta rasilimali fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa masuala ya usimamizi wa maeneo oevu ikiwemo kufanya tathmini ya uharibifu wa maeneo ya ardhi oevu; na Kuboresha

mbinu za utoaji elimu ya mazingira hususan elimu ya utunzaji wa maeneo ya ardhi oevu.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mkutano huu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Wataalam wa Nchi wanachama wa Mkataba kwa nchi zilizopo Mashariki ya Bara la Afrika na mjumbe katika kikosi kazi cha kutathmini Miji yenye hadhi ya kuitwa 'Miji yenye hifadhi ya maeneo ya ardhi oevu'.

### iv) Mkutano wa Saba (7) wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEA-7) uliofanyika Nairobi, Kenya, kuanzia tarehe 1 hadi 12 Desemba, 2025. Ujumbe wa Tanzania katika mkutano huo uliongozwa na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu, Hayati **William Vangimembe Lukuvi (Mb.),** (Mungu amrehemu) ambaye alimwakilisha **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo ni pamoja na nchi wanachama: Kujenga uwezo wa nchi kukabiliana na viumbe vamizi, kuimarisha ustahimilivu wa miamba ya matumbawe, uhifadhi wa barafu ikiwemo Mlima Kilimanjaro, na udhibiti wa moto holela; Kukabiliana na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya madawa na udhibiti wa kemikali na taka; na Kuhakikisha Matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira na matumizi ya Akili Unde katika hifadhi ya mazingira. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo ulimpitisha Mhandisi **Hamad Yussuf Masauni (Mb.),** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuwa Makamu wa Rais wa Mkutano wa nane (8) wa Baraza la Mazingira Duniani (UNEA-8).



***Aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Festo Dugange (kushoto) akimwakilisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni kushiriki Mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEA-7) uliofanyika jijini Nairobi, Kenya Desemba 11, 2025.***

### v) Mkutano wa sita (6) wa nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa sita (6) wa nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki. Mkutano huo ulifanyika tarehe 03 hadi 07, Novemba, 2025 Geneva, Uswisi. Mojawapo ya azimio muhimu katika Mkutano huu ni nchi wanachama  kukubaliana kwa pamoja kusitisha


matumizi ya zebaki kama kiambata cha dawa ya kuzibia meno (Dental Amalgam) ifikapo mwaka 2034 ili kulinda afya ya binadamu na mazingira. Aidha, Tanzania ilianza matumizi mbadala ya zebaki katika matibabu ya meno kabla ya kufikiwa kwa azimio hili.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maazimio mengine yaliyoafikiwa katika mkutano huo ni pamoja na Nchi wanachama: Kushirikiana kukomesha biashara haramu ya zebaki; Kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu; Kuhakikisha kuwa uchafuzi utokanao na zebaki hauzidi kiwango cha 15mg/kg; na Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mkataba kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025 ambapo Tanzania imewasilisha taarifa husika kwa Sekretarieti ya Mkataba.

### vi) Mkutano wa 13 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa nchi katika Mkutano wa 13 wa Mawaziri wa Nchi

Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika uliofanyika tarehe 13 hadi 17 Oktoba, 2025 Lusaka, Zambia. Maazimio yatokanayo na Mkutano huo ni pamoja na: Nchi wanachama kutekeleza azimio la kusitisha kwa muda shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu (3) ili kuweka mazingira ya utulivu kiikolojia kuwezesha kuzaliana kwa viumbe maji na kuongezeka kwa rasilimali za uvuvi; Kukamilisha taratibu stahiki za uridhiaji wa itifaki ya Ufugaji wa samaki na viumbe maji katika Ziwa Tanganyika; na Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 14 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika utakaofanyika Oktoba, 2026 Jijini Dar es Salaam. Aidha, Mkutano huo ulimpitisha Dkt. Emma Liwenga ambaye ni Mtanzania kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya kikanda chini ya mkataba husika kwa kipindi cha miaka mitatu (2026-2029).



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Richard Muyungi (kushoto) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, Dkt. Emma Liwenga, Februari 24, 2026 baada ya kufanya mazungumzo na kumpongeza kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo.*

### h) Utekelezaji wa Nguzo ya Dira 2050 Kuhusu Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais imejipanga kutekeleza Dira 2050 ipasavyo hususan Nguzo ya tatu kuhusu Uhifadhi ya Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ambapo imeandaa Mpango Mkakati wa Ofisi wa mwaka 2026 - 2030. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania yenye lengo la kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya Tabianchi kwa kuongeza eneo lenye uoto wa kijani kupitia upandaji miti na usimamizi wa mazingira.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Programu hii ni nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Dira 2050 ambayo pamoja na masuala mengine itahamasisha uhifadhi wa mazingira kama ajenda ya kitaifa, itakuwa shirikishi hasa katika ngazi ya jamii, itajenga hamasa na mwamko wa kipekee nchini na itasimamiwa moja kwa moja na Viongozi Wakuu wa Serikali ili kuipa kipaumbele katika mipango ya maendeleo katika ngazi zote. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele katika Programu hii ni pamoja na:- Kuhamasisha jamii na wadau katika kupanda na kutunza miti bilioni 2 na hekta 100,000 za bustani za kijani kwa mwaka; Kuwezesha urejeshwaji na uhifadhi wa ardhi ya kilimo, ardhi-oevu, misitu, na nyanda za malisho zilizoharibiwa kiasi cha hekta milioni 1 kwa mwaka; Kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa angalau Taasisi 13,000; Utekelezaji wa miradi 35 ya biashara ya kaboni katika sekta ya Usafirishaji, Misitu, na Nishati safi na Usimamizi wa Taka; na Kuchangia utekelezaji wa Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani (2023–2030) unaolenga kupanda miti Milioni 3 kila mwaka.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Programu hii inatarajiwa kuzinduliwa katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni, 2026. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa muda wao kwa ajili ya kutoa maoni yao yaliyosaidia kuboresha programu hii.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na uzinduzi wa programu hiyo, shughuli nyingine zitakazofanyika katika Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira ni pamoja na: Utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; Shughuli za kielelezo za uhifadhi wa mazingira; na Maonesho ya teknolojia na mbinu mbalimbali za uhifadhi wa mazingira zinazotekelezwa na wadau mbalimbali. Shughuli hizo zitahusisha Wizara, Idara na Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, Asasi za kiraia, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Washirika wa Maendeleo na wananchi kwa ujumla.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuutangazia umma kuwa Wiki ya

Mazingira itumike ipasavyo kama jukwaa la kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa vitendo. Wananchi wahamasishwe kushiriki katika upandaji miti, usafi wa mazingira, matumizi ya nishati safi, na kuzingatia sheria na kanuni za mazingira.

**i) Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi iliratibu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama ifuatavyo:

**i) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia, Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai Tanzania**

**109.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi imeendelea na utekelezaji wa Mradi huu unaolenga kuimarisha usimamizi jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo-ikolojia na jamii kwa ujumla nchini Tanzania. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Mradi

unatekelezwa katika Mikoa ya: Iringa (Halmashauri ya Wilaya ya Iringa); Mbeya (Halmashauri ya Wilaya za Mbeya na Mbarali); Njombe (Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe); Katavi (Halmashauri ya Wilaya za Tanganyika na Mpimbwe); na Rukwa (Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga). Kiasi cha shilingi bilioni 5.028 kilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: Ujenzi wa mfereji wa umwagiliaji; muindombinu ya kuwezesha ufugaji wenye tija; urejeshaji wa misitu na ardhi; mipango ya matumizi bora ya ardhi; na shughuli mbadala za kiuchumi ambazo ni rafiki kwa mazingira.

**ii) Mradi wa Kuanzisha Bustani ya Kijani Katika Eneo la Swaswa, Dodoma**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi imeendelea na utekelezaji wa mradi huu unaolenga kuboresha mandhari ya eneo la Bwawa la Swaswa kwa lengo la kuongeza uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, na kuwezesha kufanyika kwa shughuli za kiuchumi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani na za nje kupitia Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja

na; Kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kupata Kibali cha Mazingira; na Kupatikana kwa Mkandarasi ambaye ataanza shughuli za ujenzi.

iii) **Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea na utekelezaji wa Mradi huu unaolenga kujenga uwezo wa Kitaasisi kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya Montreal ambapo hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha shilingi milioni 250 kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zifuatazo: Kutoa mafunzo kwa maafisa wa Idara za Serikali na mawakala wa forodha katika mipaka ya Holili, Horohoro, Tunduma na Bandari ya Tanga na Dar es Salaam pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius K. Nyerere kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa vifaa na kemikali zinazoweza kusababisha uharibifu wa tabaka la ozoni

na ongezeko la joto duniani; Kutoa mafunzo kwa mafundi mchundo wa viyoyozi na majokofu kuhusu namna bora ya kuhudumia vifaa hivyo; na Ununuzi wa mashine za kunasa na kurejeleza gesi chakavu za majokofu na viyoyozi katika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya, Vyuo vya Elimu ya Ufundi stadi vya Zanzibar, Chang'ombe, Kilimanjaro, Morogoro, Kigoma, Lindi, na Arusha. Vilevile, kupitia mradi huu Ofisi imeandaa Mpango wa Taifa wa Usimamizi na uondoshaji wa kemikali chakavu nchini.

**iv) Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma**

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma. Lengo la mradi ni kuboresha mifumo ikolojia na kuimarisha ustahimilivu wa jamii dhidi ya mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma na kuchangia kuboresha mazingira. Mradi huu unatakelezwa katika Halmashauri ya Wilaya za

Kasulu, Kibondo na Kakonko. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuajiri timu ya uratibu wa mradi na Ununuzi wa vitendea kazi.

**v) Mradi wa kuimarisha jamii na mifumo ikolojia katika kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye Ukanda wa misitu ya miombo Tanzania Bara na maeneo kame ya Zanzibar.**

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi imeanza utekelezaji wa mradi huu unaolenga kupunguza na kuimarisha uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii pamoja na mifumo ikolojia kwenye ukanda wa Misitu ya Miombo Tanzania Bara na maeneo kame Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2025 hadi 2029 kwa gharama ya Dola za Marekani 4,416,210 sawa na shilingi 10,598,904,000.00, fedha kutoka Mfuko wa Dunia wa Mazingira kupitia Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO). Mradi huu unatekelezwa katika Mikoa saba, mitatu (03) ya Tanzania Bara ambayo ni Tabora (Sikonge), Katavi (Nsimbo) na Rukwa (Nkasi) na minne (04) ya Zanzibar ambayo ni Unguja Kaskazini

(Kaskazini B), Unguja Kusini (Kusini), Pemba Kaskazini (Micheweni) na Pemba Kusini (Chakechake).

**vi) Mradi wa Ujenzi wa Kuta za kuzuia Maji ya Bahari katika Fukwe za Mikindani – Mtwara na Sipwese Pemba.**

**114.** ***Mheshimiwa Spika*,** Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea na ujenzi wa kuta na Matuta kwa ajili ya kuzuia maji ya bahari kuingia kwenye makazi na mashamba pembezoni mwa fukwe za Mikindani Mtwara na Sipwese Pemba. Ofisi imepokea kiasi cha shilingi milioni 392 kwa ajili ya kukamilisha shughuli za mradi ambapo ujenzi umefikia asimilia 95 kwa upande wa Sipwese na asilimia 75 kwa upande wa Mikindani.

**vii) Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutekeleza mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Kwa mwaka 2025/26, kazi zilizofanyika ni ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II, Makazi ya Oysterbay (Dar es Salaam) na Kilimani Dodoma.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akikagua ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Mtaa wa Luthuli, Posta Jijini Dar es Salaam Januari 29, 2026.*

### 3) MASUALA YA UCHUMI WA BULUU NCHINI

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Uchumi wa Buluu ni moja ya maeneo mapya ya kimkakati yenye mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, maziwa, mito, mabwawa, maji chini ya ardhi na maeneo oevu kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, kuboresha maisha ya jamii na hifadhi ya rasilimali za Uchumi wa Buluu. Maeneo haya yana fursa kubwa za kuongeza uzalishaji, kukuza biashara na uwekezaji, kutoa ajira

kwa vijana na wanawake, kuimarisha usalama wa chakula, pamoja na kuongeza mchango wa sekta husika katika Pato la Taifa.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 imetambua sekta ya Uchumi wa Buluu kuwa ni sekta ya mageuzi katika kufikia malengo ya Dira hii. Hatua hii ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha Uchumi wa Buluu unakuwa nguzo muhimu ya uchumi shindani, jumuishi na endelevu.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 na Mkakati wake wa Utekelezaji kwa kuweka mfumo wa uratibu wa shughuli za Uchumi wa Buluu ikiwemo kuanza maandalizi ya Mpango wa Matumizi endelevu wa Maeneo ya Maji (Marine Spatial Planning - MSP).




### a. Kuratibu Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Serikali imeanzisha Kitengo cha Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Uratibu chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Hatua hii imeimarisha uratibu wa shughuli za Uchumi wa Buluu nchini na kuweka msingi wa usimamizi jumuishi wa sekta zote zenye mnasaba na

Uchumi wa Buluu.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uratibu huo kwa ngazi za kisekta, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Uchumi wa Buluu kupitia Kamati za maamuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu na Mawaziri. Vilevile, Ofisi imewateua Maafisa Viungo wa Uchumi wa Buluu katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika kurahisisha mawasiliano, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Uchumi wa Buluu nchini.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na kuanzishwa kwa mifumo hiyo ya uratibu, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi na wataalamu kwa kuwawezesha kushiriki mafunzo ya kikanda na kimataifa, ambapo wataalam watano waliwezeshwa kushiriki mafunzo kuhusu uandaaji wa Mpango wa matumizi endelevu wa Maeneo ya Maji yaliyofanyika Zanzibar tarehe 24 Novemba hadi 03 Disemba, 2025; na Kushiriki kwenye makongamano na Warsha za Uchumi wa Buluu. Lengo la hatua hizi ni kupata wataalamu wenye uwezo wa kusimamia kwa

ufanisi Mipango, Sera na Mikakati ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu nchini.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ajenda ya Uchumi wa Buluu inaeleweka vyema kwa Viongozi Wakuu wa Serikali na kusimamiwa kikamilifu, Ofisi iliratibu warsha ya mafunzo kwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, na Manaibu Makatibu Wakuu iliyofanyika tarehe 4 Desemba, 2025 kwa ajili ya kupata uelewa kuhusu fursa za kifedha zinazotolewa na Umoja wa Ulaya kupitia Taasisi zenye ithibati ya Umoja wa Mataifa na taasisi za fedha ikiwemo Benki za NMB, CRDB na KCB. Aidha, warsha hii ililenga kutoa msisitizo kwa Viongozi kufuatilia utekelezaji wa Miradi inayotekelezwa kupitia Wizara na Taasisi zao. Vilevile, wanufaika wa fursa hii ni wananchi kupitia vikundi vinavyoratibiwa na Wizara za kisekta zenye mnasaba na Uchumi wa Buluu.

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuimarisha ushirikiano wa masuala ya Uchumi wa Buluu baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Ofisi iliratibu Kikao cha Mashirikiano na Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kilichofanyika tarehe 13 Februari, 2026 ambapo mikakati ya ushirikiano iliyoafikiwa ni pamoja na:- Kuendeleza na kuratibu tafiti jumuishi za Uchumi wa Buluu kati ya SJMT na SMZ; Kufanya maandalizi na utekelezaji wa miradi ya pamoja katika shughuli za Uchumi wa Buluu; Uandaaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji (*Marine Spatial Planning – MSP*); Ushiriki wa pamoja katika Mikataba na Majukwaa ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu Uchumi wa Buluu; na Kujengeana uwezo, kubadilishana taarifa, uzoefu na mbinu bora za utekelezaji wa shughuli za Uchumi wa Buluu kwa pande zote mbili.

**b. Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji (Marine Spatial Planning - MSP)**

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa matumizi endelevu ya rasilimali za Uchumi wa Buluu, katika mwaka 2025/26 Serikali imeanza mchakato wa kuandaa Mpango wa Matumizi Endelevu wa Maeneo ya Maji. Mpango huu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha rasilimali za bahari na maji baridi zinatumika kwa tija, kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi,

kuboresha maisha ya jamii na hifadhi ya rasilimali za maji kwa lengo la kupunguza migongano ya matumizi na kufungua fursa mpya za uwekezaji.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanyika ni pamoja na: Kuandaliwa kwa Taarifa ya Tathmini ya Hali ya Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji Tanzania; Kuandaliwa kwa Mkakati wa Ushirikishwaji wa Wadau katika Kuandaa na Kutekeleza wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji wa mwaka 2026–2035; na Mpango Kazi wa Maandalizi ya Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji wa mwaka 2025–2030.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya majaribio ya uandaaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji katika Halmashauri za Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga, pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga Mkoani Pwani. Lengo la miradi hii ni kupata uzoefu wa kitaalam na kiutekelezaji utakaoisaidia nchi kuandaa kwa ufanisi Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji na kupunguza changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wake.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kutumia fursa hii kuwahimiza wadau wote kushiriki kikamilifu katika zoezi la uandaaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji, kwa kuwa huu ni mpango shirikishi utakaosaidia kuondoa migongano ya matumizi ya rasilimali zilizopo ndani ya maji, kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za Uchumi wa Buluu na kuwezesha ukuaji wa uwekezaji katika sekta mbalimbali za Uchumi wa Buluu.

### c. Elimu kwa Umma kuhusu Masuala ya Uchumi wa Buluu

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Uchumi wa Buluu kupitia vyombo vya habari, makongamano, semina, warsha na maonesho ya kitaifa na kimataifa. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuratibu Kongamano la Tatu la Kimataifa la Uchumi wa Buluu lililofanyika Jijini Dar es Salaam na kukutanisha wataalam na watafiti kutoka ndani na nje ya nchi kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kutangaza fursa za Uchumi wa Buluu.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Ofisi iliratibu na kufanikisha Kongamano la kwanza la Kitaifa la Wadau wa Uchumi wa Buluu (National Blue Economy Stakeholders Conference - NBESC) lililofanyika tarehe 10 hadi 11 Septemba, 2025 Jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lililenga kujadili fursa, changamoto na mikakati ya kuendeleza sekta ya Uchumi wa Buluu nchini pamoja na kutambua hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuimarisha sekta ya Uchumi wa Buluu.



***Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi (katikati) akiongoza Kongamano la Kitaifa la Wadau wa Uchumi wa Buluu lililofanyika jijini Dar es Salaam Septemba 10 hadi 11, 2026.***

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha elimu kuhusu Uchumi wa Buluu inawafikia wadau wengi

zaidi, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa Umma kupitia Mikutano, Semina, Warsha mbalimbali ambazo zilirushwa kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, runinga na mitandao ya kijamii ambapo elimu kuhusu fursa, umuhimu na wajibu wa kila mdau katika kukuza sekta imeendelea kutolewa kupitia kaulimbiu isemayo "Uchumi wa Buluu na Tanzania Tuitakayo".

## 4) MASUALA MENGINE YALIYOTEKELEZWA

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Ofisi kwa kipindi cha mwaka 2025/26 ni pamoja na: Kuendelea kusimamia masuala ya utawala na usimamizi wa rasilimali watu ikiwemo utoaji wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi.

## 5) BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Mipango, Miongozo na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa Serikali. Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza lilitekeleza shughuli zifuatazo:

### a) Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191

#### i) Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi,2026 Baraza lilifanya kaguzi katika miradi 3,408 ikijumuisha viwanda, migodi (yakiwemo machimbo ya mchanga na kokoto), mitambo ya gesi na mafuta na nishati ya umeme, machinjio ya wanyama, kumbi za starehe, nyumba za ibada, hoteli, mabomba ya mafuta, maghala ya kemikali na taka zenye madhara, vituo vya mafuta, masoko, madampo, hifadhi ya vyanzo vya maji, mashamba, mifumo ya maji taka, Taasisi za elimu na afya, maghala ya kuhifadhi kemikali na taka hatarishi, majengo ya biashara na makazi pamoja na miradi mingine ya maendeleo nchini.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya kaguzi hizo ni pamoja na kuongezeka kwa uzingatiaji wa Sheria na ubora katika hifadhi ya mazingira kwa maeneo yote yaliyokaguliwa. Hii imetokana na ongezeko la utoaji elimu na ushauri kuhusu uhifadhi wa mazingira na

uzingatiaji, uwekaji mifumo thabiti ya kuhifadhi taka ngumu, kuboresha mifumo ya kutibu majitaka na udhibiti wa hewa chafu. Hata hivyo, miradi 137 sawa na 4% ya miradi iliyokaguliwa ilibainika kutozingatia sheria na hivyo wahusika walichukuliwa hatua stahiki za kisheria. Kutokana na kaguzi hizo, kumekuwa na ongezeko la wawekezaji wanaojisajili kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kaguzi za mazingira kutokana na uhamasishaji na ufuatiliaji unaofanyika.



***Watalaam wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ilala jijini Dar es Salaam, Februari 25, 2026 wakifanya ukaguzi wa mazingira pamoja na kutoa elimu ya Uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira viwandani.***

### i) Udhibiti wa Taka Hatarishi

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza limeendelea kusimamia utekelezaji

wa Kanuni za Udhibiti wa Taka Hatarishi za mwaka 2019 na marekebisho yake ya mwaka 2021. Katika kipindi hicho, jumla ya maombi 224 ya vibali vya usimamizi wa taka hatarishi yalipokelewa, ambapo vibali 212 vilitolewa sawa na asilimia 95. Vilevile, Baraza lilipokea maombi 28 ya uteketezaji wa taka hatarishi na kusimamia uteketezaji na udhibiti wake ambapo kiasi cha tani 15,572.7 ziliteketezwa. Taka hizo ni pamoja na:- Dawa zilizokwisha muda wake, vifaa tiba vilivyokwisha muda wake pamoja na mabati ya ASBESTOS.

**136.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kupitia Bunge lako Tukufu, niwakumbushe watu binafsi na Makampuni yanayojihusisha na biashara ya taka hatarishi kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizopo ili kutunza mazingira.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Kanuni ya Kupiga Marufuku Matumizi ya Mifuko ya Plastiki, Baraza limeendelea kudhibiti matumizi ya mifuko hiyo, ambapo hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya tani 60 zimekamatwa na kati ya hizo tani 40 zimeteketezwa na tani 20 zilizobaki zinasubiri taratibu za kuteketezwa.



***Watumishi kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ziwa Victoria Mashariki kwa kushirikiana na Mamlaka za Ulinzi na Usalama wakiwa wamekusanya mifuko ya plastiki iliyokamatwa na kuhifadhiwa katika vituo mbalimbali vya polisi baada ya kesi zake kukamilika kisheria, zoezi lililofanyika kuanzia Februari 13, 2026.***

## ii) Kushughulikia Malalamiko ya Umma Kuhusu Uchafuzi na Uharibifu wa Mazingira

**138.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza limeshughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake. Hadi Machi, 2026, Baraza limepokea jumla ya malalamiko 179 kuhusu masuala mbalimbali ya kimazingira, ikiwemo kelele zilizozidi

viwango vilivyowekwa. Kati ya hayo, malalamiko 162 sawa na asilimia 91 yalishughulikiwa ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu kwa walalamikiwa waliotenda makosa kwa mujibu wa sheria na kanuni za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

**b) Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira**

**i) Miradi Iliyosajiliwa**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kusimamia usajili wa miradi ya maendeleo kwa ajili ya kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira ambapo jumla ya Miradi 1,471 ilisajiliwa. Kati ya hiyo, miradi 1,180 ilisajiliwa kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na miradi 291 kwa ajili ya Ukaguzi wa Mazingira. Kwa kipindi hicho, jumla ya miradi ipatayo 1,030 imeidhinishwa kupata vyeti ambapo miradi 903 ni ya tathmini ya athari kwa mazingira na 127 ni miradi ya ukaguzi wa mazingira.

### c) Usajili na Uratibu wa Utendaji Kazi wa Wataalam Elekezi wa Mazingira

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza limesajili na kutoa vyeti vya utendaji kazi kwa wataalam elekezi wa mazingira. Hadi Machi, 2026, Baraza limepokea na kuchakata jumla ya maombi 453 ya usajili, vyeti vya utendaji kazi wa wataalam elekezi wa mazingira pamoja na uhuishaji wa vyeti vya utendaji kazi wa wataalam elekezi wa mazingira (Usajili 147, Utendaji 120 na uhuishaji 186). Kati ya maombi hayo, jumla ya wataalam elekezi wa mazingira 51 walioomba usajili waliidhinishwa na Bodi na orodha kuwasilishwa kwenye mamlaka husika. Vilevile, Baraza lilitoa vyeti 193 vya usajili na utendaji kazi wa wataalam elekezi wa mazingira.

### d) Utekelezaji wa Ajenda ya Taifa ya Tafiti za Mazingira (Tafiti na Tathmini)

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Mazingira (NERA) yenye lengo la kutoa mwelekeo wa kitaifa kwa wadau wa kufanya tafiti za mazingira ili kuwawezesha

kuandaa programu, miradi na shughuli mbalimbali za kitafiti kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele ya Kitaifa yaliyomo kwenye ajenda na Dira ya Taifa ya Maendeleo, DIRA 2050.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** warsha kwa ajili ya kupitia rasimu ya NERA ya mwaka 2026–2036 ilifanyika Mkoani Morogoro kuanzia tarehe 29 hadi 30, Januari, 2026 ikijumuisha Kamati ya Taifa ya tafiti za Mazingira. Aidha, NERA imeidhinishwa na Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kupitia Ajenda hii, Baraza linaratibu utekelezaji wa tafiti na miradi ya mazingira kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele sambamba na masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira yaliyoainishwa kwenye DIRA 2050.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ajenda iliyoandaliwa imezingatia jukumu la tafiti za mazingira na tathmini ya mifumo ikolojia. Maeneo ya kipaumbele ya tafiti ni pamoja na: Usimamizi wa taka na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira; Uhifadhi na Usimamizi Jumuishi wa rasilimali za maji; Usimamzi wa matumizi ya ardhi; Uhifadhi wa Bioanuai; Uhimilivu na kukabiliana na

athari za mabadiliko ya tabianchi; Usimamizi wa masuala ya kijenetiki; na Matumizi ya teknolojia katika usimamizi wa mazingira na maendeleo ya uchumi na mazingira.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha uwezo wa nchi wa utafutaji wa rasilimali fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Baraza limefanya jitihada za kuhuisha Ithibati ili kuwezesha kupata fedha kupitia Mfuko wa kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund). Katika hatua hii, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Baraza limefanikiwa kukamilisha hatua hii na hivyo kukidhi vigezo vya kupokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za maporomoko ya ardhi ambazo zimekuwa zikijitokeza katika maeneo mbalimbali hapa nchini kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, Baraza limefanya jitihada ya kuainisha maeneo yenye changamoto hususan katika maeneo ya milima na

kufanya tathmini ya mifumo ikolojia ili kubaini njia sahihi ya kukabiliana na changamoto hizo. Hadi kufikia Machi, 2026 Baraza limefanya tathmini kwenye milima ya Kawetere na Livingstone (Mbeya), milima ya Mambamiamba (Kilimanjaro) na safu za milima ya Chinyami (Dodoma). Aidha, tathmini hizo zitatumika kuandaa mipango ya usimamizi wa mazingira kwenye maeneo hayo. Vilevile, uandaaji wa Mpango jumuishi wa usimamizi wa mazingira wa mlima Kawetere umekamilika.

### e) Uandaaji Maandiko Dhana na Mapendekezo ya Miradi

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kuandaa maandiko mbalimbali ya miradi kwa ajili ya kutafuta fedha za kusaidia shughuli za kuhifadhi mazingira. Hadi kufikia Machi, 2026, Baraza limeandaa maandiko saba (7) ikijumuisha maandiko kamili ya miradi minne (4) pamoja na maandiko dhana matatu (3). Maandiko hayo yamejikita zaidi katika eneo la Mabadiliko ya tabianchi.

### f) Kuandaa Nyenzo na Miongozo ya Mazingira

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeandaa Mwongozo unaosaidia katika ukusanyaji wa taarifa za taka zinazozalishwa viwandani. Mwongozo huu ni mahsusi katika kusaidia utambuzi, ukusanyaji wa takwimu, uainishaji na uwasilishaji wa taarifa za taka za viwandani.

### g) Uratibu na Matokeo ya Miradi inayotekelezwa na Baraza

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuratibu miradi mbalimbali ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwemo mradi wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Madini ya Dhahabu ambapo shughuli zifuatazo zimefanyika:- Ujenzi wa kituo cha teknolojia mbadala wa zebaki, Kata ya Msalala Wilaya ya Kahama Shinyanga; Ujenzi wa mialo 8 ya mfano ya uchenjuaji salama kwa kutumia zebaki katika mikoa ya Geita, Mwanza, Singida, Shinyanga na Mbeya; na ujenzi wa kituo cha elimu kuhusu zebaki katika Mkoa wa Geita. Ujenzi huu

wa kituo cha elimu umekamilika kwa asilimia 90. Vilevile, mradi huu umesaidia kuimarisha maabara za taasisi nne (4) ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Tume ya Madini; na Taasisi ya Jiolojia na Tafiti za Madini nchini. Pamoja na matokeo hayo, mradi huu umetoa elimu ya matumizi salama ya zebaki, athari zake katika afya ya jamii na teknolojia mbadala kwa zaidi asilimia 30 ya wachimbaji wadogo nchini.

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limetekeleza mradi wa kujenga uwezo wa Taifa wa kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, EMA, kwa kununua gari lenye vifaa vya maabara *(Mobile Laboratory).* Gari hili lina vifaa vya kusaidia kuchukua sampuli na kufanya vipimo vya ubora wa hewa na maji katika maeneo husika. Vilevile, Baraza linasimamia utekelezaji wa miradi minne (4) ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambapo miradi hii inatekelezwa na wadau mbalimbali nchini. Lengo la miradi hiyo ni kuongoa mifumo ya ikolojia na kukabiliana na athari za mabadiliko ya

tabianchi katika mikoa ya Kaskazini Unguja (Kaskazini B), Pemba Kaskazini (Wete), Dodoma (Kongwa na Bahi); Singida (Manyoni); Tabora (Nzega na Igunga); na Mara (Bunda).




***Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Semesi (katikati mwenye miwani) akipokea mfano wa ufunguo kama ishara ya makabidhiano ya maabara inayotembea iliyofadhiliwa na Serikali ya Sweden katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam Februari 19, 2026.***

### h) Elimu kwa Umma

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza limefanikiwa kuendesha programu 78 za mazingira kupitia redio jamii na taifa, programu 52 za runinga, makala maalumu tatu (3) za televisheni, habari 151 za runinga, habari 109 za redio na taarifa 563 zilisambazwa katika mitandao mbalimbali ya

kijamii. Aidha, habari 278 zilichapishwa kwenye magazeti, vipeperushi 384 vya kielektroniki vyenye jumbe za mazingira vimeandaliwa na kuhuishwa kwenye mitandao ya kijamii ya NEMC, picha mjongeo 26 na mikutano sita (6) ya waandishi wa habari.



***Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Semesi akifafanua jambo wakati wa kikao cha uwasilishwaji wa Taarifa ya Bajeti kwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, jijini Dodoma Machi 23, 2026.***

## 6) KITUO CHA TAIFA CHA KURATIBU KABONI

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Kitaifa cha Kuratibu Kaboni, kimeanzishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 iliyofanyiwa marekebisho kupitia Sheria Namba Na. 5 ya Mwaka 2025 na kupewa Majukumu ya: Kuratibu masuala

yanayohusiana na gesijoto na Biashara ya Kaboni; Kuwa Msajili wa miradi ya kaboni; Kuweka Mfumo wa Ufuatiliaji, Utoaji wa Taarifa na Uthibitishaji wa Gesijoto; Kutoa Mafunzo na uhamasishaji kwa wadau, Kufuatilia utekelezaji wa Kanuni za Biashara ya Kaboni; na Kuweka Mipango ya kukuza uwekezaji na ushirikiano wa kimataifa katika Biashara ya Kaboni nchini.



***Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi Baraka Luvanda (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji Kaboni (NCMC), Bi. Kathryn Kigaraba pamoja na Watendaji wa Kituo hicho wakati wa ziara ya kikazi kituoni hapo mkoani Morogoro Machi 04, 2026.***

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni, kimeendelea kuratibu na kuimarisha usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026

shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Muundo na Majukumu ya Kituo sambamba na Uratibu wa Biashara ya Kaboni yalifanyika tarehe 19 Januari, 2026 katika ukumbi wa Bunge Dodoma; Kuwajengea uwezo wa kufanya biashara ya Kaboni taasisi na wadau mbalimbali ikiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Aidha, elimu kwa umma kuhusu biashara ya kaboni imeendelea kutolewa kupitia njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Kituo kilitekeleza shughuli zifuatazo: Usajili wa miradi 22 ya Biashara ya Kaboni ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na hivyo idadi ya miradi iliyosajiliwa kufikia 99. Miradi hiyo imegawanyika katika sekta mbalimbali, ambapo asilimia 49.5 ipo katika sekta ya Misitu, asilimia 40.4 katika sekta ya Nishati, asilimia 3 katika sekta ya Kilimo, asilimia 2 katika sekta ya udhibiti wa taka, na asilimia 1 sekta nyingine.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2026 halmashauri 24 kati ya 184 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa biashara ya kaboni. Halmashauri nne (4) za Tanganyika, Kiteto, Karatu na Mbulu zinapokea fedha kwa ajili ya utekelezaji miradi ya maendeleo; Halmashauri sita (7) za Bukoba, Misenyi, Muleba, Ngara, Karagwe,kyerwa na Biharamulo fedha za biashara ya kaboni hutolewa kwa wananchi moja kwa moja ambapo wananchi 16,908 wananufaika; na halmashauri 13 za Mpwapwa, Kilosa, Liwale, Gairo, Kongwa, Tunduru, Mvomero, Morogoro, Longido, Monduli, Namtumbo, Kilolo na Monduli ziko kwenye hatua mbalimbali kwa kufanya tathimini na kuandaa maandiko ili kuendelea na biashara ya kaboni kwa mwaka 2026/27.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa wito kwa Halmashauri zote nchini kukitumia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni kwa ajili ya ushauri, uratibu na usimamizi wa miradi ya kaboni ili kuhakikisha miradi hiyo inazingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa, inaleta manufaa halisi kwa wananchi, na inalinda rasilimali za mazingira kwa uendelevu. Aidha, Halmashauri zinahimizwa kushirikiana kikamilifu na

wadau mbalimbali wakiwemo sekta binafsi na jamii za wananchi ili kuongeza wigo wa miradi ya kaboni, kuimarisha uwazi katika mikataba, na kuhakikisha mapato yanayotokana na biashara ya kaboni yanachangia ipasavyo katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa biashara ya kaboni inaendeshwa kwa uwazi na fursa zilizopo zinatumika ipasavyo na kuleta tija na manufaa kwa wananchi, Serikali iliunda Kamati ya Wataalamu iliyopewa majukumu ya kushauri kuhusu mikakati madhubuti ya kuimarisha usimamizi wa biashara ya kaboni; kubaini na kutoa mapendekezo ya kushughulikia changamoto zilizopo au zinazoweza kujitokeza katika biashara ya kaboni.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi, ikiwemo kuimarisha mifumo ya kidijitali ya usajili na ufuatiliaji wa miradi, kujenga uwezo kwa wataalam wa halmashauri, na kuhakikisha kuwa biashara ya kaboni inakuwa chachu ya ukuaji wa uchumi wa Taifa, uhifadhi wa mazingira, na ustawi wa wananchi wetu.

**158.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na ukweli kuwa Biashara ya Kaboni ni dhana ngeni kwa wananchi, ninaomba nitoe rai kwa umma kutumia ipasavyo Kituo cha Uratibu wa Kaboni nchini ili kupata ushauri wa kitaalamu na miongozo stahiki kuhusu biashara hiyo ikiwa ni pamoja na uandaaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye fursa ya biashara ya Kaboni ambayo siyo tu inachangia ukuaji wa uchumi lakini pia uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



***Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC) Bi. Kathryrn Kigaraba akifafanua jambo wakati wa kikao cha uwasilishaji wa taarifa kuhusu muundo na majukumu ya NCMC kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, jijini Dodoma Januari 19, 2025.***

## 7) CHANGAMOTO NA UTATUZI

### a) Changamoto

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** mbali na mafanikio makubwa yaliyopatika katika mwaka 2025/26, Ofisi ilipitia changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na: Uelewa mdogo wa masuala yanayohusu chimbuko, misingi, historia na fursa za Muungano. Hii inatokana na uhalisia kuwa idadi ya watu waliozaliwa baada ya Muungano ni zaidi ya asilimia 75.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa hifadhi na usimamizi wa Mazingira changamoto zilizopo ni pamoja na: Jamii kutozingatia kikamilifu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake; Uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi na biashara ya kaboni; Uwepo wa mnyororo mrefu wa biashara ya kaboni unaojumuisha madalali wengi na kusababisha kupungua kwa mapato halisi; Utegemezi mkubwa wa rasilimali za mazingira kwa baadhi ya jamii nchini katika kujipatia kipato na kujikimu bila kuzingatia hifadhi ya mazingira.

**161. Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine ni ukosefu wa Mpango wa Matumzi Endelevu ya Maeneo ya Maji (MSP) kunakosababisha kutonufaika vyema na fursa zilizopo katika sekta za Uchumi wa Buluu; na uelewa mdogo wa jamii kuhusu fursa za Uchumi wa Buluu na namna ya kunufaika nazo; na kuongezeka kwa matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za Uchumi wa Buluu kunakosababisha uharibifu wa rasilimali za maji.

### a) Utatuzi wa Changamoto

**162.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na Changamoto hizo kwa mwaka 2025/26, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano na fursa zake, uzalendo na mshikamano wa Kitaifa hususan kwa vijana. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na: Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa Mazingira hususan uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake pamoja na biashara ya kaboni; na Kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uhifadhi na

usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira limeendelea kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa miradi inayokiuka taratibu zilizowekwa. Kuanzisha rejesta ya kidijitali na mifumo ya kisasa ya upimaji, utoaji na uthibitishaji wa taarifa ili kuongeza uwazi, ufanisi na kuimarisha nafasi ya nchi katika soko la kaboni kimataifa.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kukamilika kwa utafiti wa awali kuhusu maandalizi ya mpango wa matumizi endelevu wa maeneo ya maji; Kukamilika kwa nyenzo zitakazotumika kuandaa MSP ikiwemo Mwongozo wa Mpango wa Matumizi ya Rasilimali za Maji, Mkakati wa Ushirikishwaji Jamii katika Uandaaji wa MSP; Kuandaa mpango wa kitaifa utakaosaidia katika uandaaji MSP; Kufanyika kwa miradi ya majaribio ya upangaji wa maeneo ya maji katika Halmashauri za Wilaya ya Mkinga (Tanga) na Mkuranga (Pwani); na kutoa elimu kwa jamii kuhusu fursa zilizopo katika sekta za Uchumi wa Buluu.

## D. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

**164.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Mpango na bajeti ya Ofisi kwa mwaka 2026/27 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: DIRA 2050; Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31); Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021; Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024; Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025; Mpango Mkakati wa Ofisi (2026/27 - 2030/31); Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/27; Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi; na Maagizo ya Viongozi wa Kitaifa.

## E. SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA OFISI KWA MWAKA 2026/27

### 1) MASUALA YA MUUNGANO

**165.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2026/27, Ofisi itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kwa masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuendelea na utekelezaji wa mpango Kabambe wa Elimu kwa umma kuhusu Muungano ambao pia unahusisha maandalizi ya ujenzi wa vituo vya Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano (MAKAVAZI) na Msafara wa Muungano (Muungano Caravan); Kuendeleza tafiti kuhusu uelewa wa Vijana katika masuala ya Muungano Tanzania Bara na Zanzibar; Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zinazotekelezwa pande mbili za Muungano; Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano ikiwemo kukamilisha utatuzi wa hoja za Muungano na kuhamasisha fursa za Muungano;

Kuratibu Vikao vya ushirikiano baina ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za SJMT na SMZ; Kufanya ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Masuala 22 ya Muungano; Kuandaa Maadhimisho ya Miaka 63 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na Kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Jimbo; Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Zanzibar; na Watendaji wa Halmashauri kuhusu uendeshaji na usimamizi wa fedha za Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.

### 2) HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

**166.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha mwaka 2026/27, Ofisi imepanga kuratibu na kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuratibu utekelezaji wa Dira ya 2050 katika masuala yanayohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ikiwemo utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania; Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Kuratibu Utekelezaji wa Mpango Kabambe

wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032); Kuimarisha uratibu na utekelezaji wa masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Wizara za Kisekta, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali wa mazingira ikiwemo kuimarisha upatikanaji wa taarifa kupitia mifumo ya kielektroniki; Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira; na Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Hifadhi ya mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka huu Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 12 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi. Mkutano huo unategemewa kufanyika tarehe 06 - 09 Oktoba, 2026 Jijini Dar es Salaam. Aidha, Mkutano huo unatarajiwa kuleta manufaa katika nyanja mbalimbali ikiwemo kupata fursa za miradi na uwekezaji; kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa; na kutangaza bidhaa mbalimbali za kiasili zinazotengenezwa hapa nchini.

### 3) URATIBU WA SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU

**168.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika kutekeleza Dira 2050, Ofisi itaendelea kuratibu na kusimamia sekta zenye mnasaba na Uchumi wa Buluu ili kuhakikisha Malengo yaliyokusudiwa na Dira 2050 yanafikiwa kwa kuweka mazingira wezeshi ya Uwekezaji katika sekta ya Uchumi wa Buluu.

**169.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2026/27, Ofisi itaendelea kuimarisha mfumo wa uratibu wa shughuli za Uchumi wa Buluu kwa kuandaa Mwongozo wa uratibu pamoja na kuandaa Mpango Kabambe wa Uwekezaji katika sekta za Uchumi wa Buluu (Blue Economy Investment Masterplan) ili kuwezesha utekelezaji madhubuti wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 na Mkakati wake wa Utekelezaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa sekta ya Uchumi wa Buluu inachangia kikamilifu kwenye Pato la Taifa.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpangokazi wa Maandalizi wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji (2025-2030), Ofisi

imejipanga kuanza na Maeneo ya Kitaifa ya maji bahari (Territerial Water) ambapo kwa mwaka 2026/27, Ofisi itaratibu maandalizi ya Mpango kwa kukusanya takwimu na taarifa za msingi, kufanya tathmini ya kiikolojia na kutambua matumizi ya kibinadamu katika maeneo ya maji, pamoja na kuendesha kampeni za elimu kwa umma na uhamasishaji kuhusu mpango huo. Kukamilika kwa mpango huu kunatarajiwa kuongeza mchango wa sekta ya Uchumi wa Buluu katika Pato la Taifa, ikiwemo kukuza uchumi wa Nchi, kuboresha maisha ya jamii, kuhifadhi rasilimali za Uchumi wa Buluu katika kupanua wigo wa ajira na kupunguza migongano ya matumizi ya rasilimali za maji kwa wanufaika.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu masuala ya Uchumi wa Buluu kupitia makongamano ya kitaifa na kimataifa ya wadau wa Uchumi wa Buluu; Kujenga uwezo wa watalaam kuhusu Uchumi wa Buluu; Kuratibu programu za elimu kwa umma kwa wadau mbalimbali ikiwemo Kamati za Bunge, Wizara,

Mamlaka za Serikali za Mitaa na jamii kwa ujumla.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2026/27, Ofisi itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta za Uchumi wa Buluu kwa kutumia utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuongeza mitaji, teknolojia, ubunifu na ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

### 4) KAZI NYINGINE ZITAKAZOTEKELEZWA NA OFISI

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi kwa mwaka 2026/27 ni pamoja na: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza majukumu yake; Kusimamia masuala ya Utawala na Menejimenti ya Rasilimaliwatu; Kuratibu maandalizi ya maandiko na nyaraka mbalimbali za Ofisi; Kuandaa Mpango na Bajeti ya Ofisi na taarifa za utekelezaji wa mipango mbalimbali; Kuelimisha umma kuhusu Majukumu, Sera, Mikakati na Programu zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais; Kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria; Kufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake; Kusimamia

utekelezaji wa mifumo ya manunuzi na kutoa taarifa; Kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya Fungu 26 na 31; Kufanya Ufuatiliaji na Tathimini ya utekelezaji wa Sera, Mikakati, Mikataba ya Kimataifa pamoja na Programu zinazohusu Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu; na Kuandaa, Kusimamia Mifumo na Kutoa Msaada wa Kitaalamu katika masuala ya TEHAMA.

## 5) KURATIBU UTEKELEZAJI WA MIRADI NA SHUGHULI WEZESHI ZA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

### a) Utekelezaji wa Miradi

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mwaka 2026/27, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama ifuatavyo:

#### i. Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo kuu la mradi ni kuimarisha usimamizi jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo-ikolojia na jamii kwa ujumla nchini

Tanzania. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2026/27 ni pamoja na: Kujenga miundombinu ya mifugo ikiwemo majosho, mabirika, na mabanio katika Halmashauri saba (7) zinazotekeleza mradi ambazo ni Mbeya, Iringa, Tanganyika, Mpimbwe, Sumbawanga, Wanging'ombe na Mbarali; Kununua na kufunga mifumo ya gesi ya kupikia katika Halmashauri tano (5) za Wilaya (Mbeya, Iringa, Tanganyika, Mpimbwe na Sumbawanga); Kukamilisha ununuzi na uwekaji wa mitambo ya uchakataji wa mazao kwa ajili ya kuongeza thamani katika viwanda vidogo sita katika Halmashauri za Iringa, Wanging'ombe, Mbarali, Sumbawanga, Mpimbwe, na Tanganyika; na Kuanzisha vitalu saba (7) vyenye jumla ya miche 2,100,000 katika Halmashauri saba (07) za Wilaya (Mbeya, Iringa, Tanganyika, Mpimbwe, Sumbawanga, Wanging'ombe na Mbarali).

### ii. Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuboresha mifumo ikolojia itakayoongeza ustahimilivu

wa mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma na hivyo kuchangia moja kwa moja kuboresha mazingira katika eneo husika. Katika mwaka 2026/27 shughuli za mradi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: Kuandaa Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji 20; Kufanya tathmini ya migogoro ya ardhi na kubuni mbinu za kupunguza migogoro hiyo; Kuainisha na kupima maeneo kwa ajili ya kupanda miti; Kujenga miundombinu ya uvunaji maji na kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za umwagiliaji; Kuotesha miti hekari 12,000 kwa njia ya kilimo mseto; Kufanya manunuzi ya vifaa na vitendea kazi vya Ofisi; Kujenga miundombinu ya kudhibiti mafuriko na mmomonyoko wa ardhi katika maeneo yenye idadi kubwa ya watu ili kupunguza athari na kuhifadhi mazingira; Kutekeleza Mipango ya Usimamizi Shirikishi ya Misitu ya Jamii; Kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi na kilimo kinachohifadhi mazingira na ufugaji wa nyuki; Kutoa mafunzo kwa Viongozi wa Vijijiji, Kata na Wilaya kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi; na Kutoa elimu kwa wakulima, Maafisa Ugani wa Wilaya kuhusu kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi.

iii. **Mradi wa kuimarisha jamii na mifumo ikolojia katika kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye Ukanda wa misitu ya Miombo Tanzania Bara na maeneo kame Zanzibar**

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kupunguza athari na kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika jamii zinazozunguka maeneo ya misitu ya Miombo Tanzania Bara na maeneo kame Zanzibar. Katika mwaka 2026/27 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: Ununuzi wa vifaa vya kuchakata, kufungasha na kutunza malisho ya mifugo na mbegu katika maeneo ya utekelezaji wa mradi; Kujenga jengo kwa ajili ya kukusanya, kuchakata na kuzalisha mbegu za miti na mazao; Kujenga manzuki kwa ajili ya kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya nyuki; na Kuanzisha vitalu vya miti katika ngazi ya vijiji upande wa Tanzania Bara; na Kufanya Mapitio ya Mkakati wa Mazao yasiyo ya Mbao Zanzibar.

### iv. Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Babati

**178.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Lengo la mradi huu ni kurejesha ikolojia ya Ziwa Babati lililoathiriwa kutokana na shughuli za kibinadamu. Katika mwaka 2026/27 shughuli zitakazotekelezwa zinajumuisha:- Kubaini na kuweka mipaka ya kudumu katika ziwa; Kupanda miti ili kuzuia mmomonyoko wa udongo; Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Matumizi wa rasilimali za Maji; Kubainisha shughuli mbadala za kujikimu kwa jamii zinazozunguka maeneo ya ziwa; na Kutoa mafunzo kuhusu udhibiti wa magugu maji kwa jamii zinazozunguka eneo la ziwa.

### v. Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Chala na Ziwa Jipe

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuimarisha ikolojia na usimamizi endelevu wa Ziwa Chala na Ziwa Jipe. Katika mwaka 2026/27 shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kuhamasisha mbinu za asili zinazotumika kuondoa magugu maji katika Ziwa Chala na Ziwa Jipe; Kufanya mapitio ya sheria

ndogo zinazosimamia Ziwa Chala na Jipe; Kubainisha njia mbadala za kujikimu kwa jamii zinazozunguka katika maeneo ya ziwa; na Kukuza uelewa wa jamii kuhusu usimamizi endelevu wa Ziwa.

### vi. Mradi wa Bustani ya Kijani Katika Eneo la Swaswa Mnarani, Dodoma

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuanzisha eneo lenye mandhari ya kijani na mazingira safi katika eneo oevu la Swaswa Mnarani Jijini Dodoma. Kwa kipindi cha mwaka 2026/27 shughuli zitakazotekelezwa ni:- Kuwezesha uchimbaji wa kisima kimoja; Kuweka miundombinu; na Kuwezesha ujenzi wa jengo la kupumzika na Bwalo la Chakula.

### vii. Program ya kujenga uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (SCALE)

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** Program hii inatekelezwa katika Halmashauri 65 (54 Tanzania bara na 11 Zanzibar). Baadhi ya Halmashauri hizo ni pamoja na: Buhigwe, Nsimbo, Chemba, Kilolo, Chake Chake, Mkoani, Kaskazini A, na Kaskazini B. Programu hii

inatekelezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Lengo la progamu hii ni kujenga uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kupitia programu hii jamii itahusika moja kwa moja katika kuibua miradi mahsusi inayolenga kutatua changamoto za mazingira na kuongeza uhimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi zilizojitokeza katika maeneo yao. Kwa kipindi cha mwaka 2026/27 kazi zilizopangwa kutekelezwa zinajumuisha: Ununuzi wa gari moja kwa ajili ya mradi; Kuandaa na kufanya mapitio ya Miongozo na Mikakati mbalimbali ikiwemo Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi; Kujenga uwezo wa jamii kuhusu uibuaji na uandaaji wa miradi ya mabadiliko ya tabianchi; Ukusanyaji wa takwimu za mabadiliko ya tabianchi na uandaaji wa taarifa; Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya Serikali za Mitaa zinazotekeleza program; na Kujenga uwezo kwa Halmashauri 54 kuhusu nyenzo za mazingira katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### viii. Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza uoto wa kijani kupitia upandaji miti na kuboresha usimamizi wa mazingira. Kwa mwaka 2026/27 shughuli zilizopangwa ni kuwezesha wadau mbalimbali na jamii kuotesha na kutunza miti bilioni 2 na kuanzisha hekta 10,000 za sehemu za kijani (green parks).

### b) Utekelezaji wa Shughuli Wezeshi

### i. Kujenga Uwezo wa Kitaifa wa Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi

**183.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/27 shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa: Kuandaa Taarifa ya awali itakayobainisha wadau, mpangilio wa kitaasisi na mifumo ya kisheria kuhusu mabadiliko ya tabianchi na Warsha ya wadau kwa ajili ya kupitia taarifa hiyo; Kuwezesha mfumo wa kitaifa wa ukusanyaji wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi

utakaojumuisha moduli za uzalishaji wa gesijoto (GHG Inventory), ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mchango ya Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (NDC) pamoja na taarifa za fedha za mabadiliko ya tabianchi; Kuratibu warsha mbili (2) za mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya kutumia mfumo wa kitaifa wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi; na Kufanya manunuzi ya vifaa vya Ofisi.

**ii. Kujenga Uwezo wa Kitaasisi Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni**

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Ofisi imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: Kufanya mafunzo kwa mawakala wa forodha 200 na watekelezaji wengine wa sheria; Kufanya mafunzo kwa Mafundi mchundo 250 wa viyoyozi na majokofu kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo bila kuathiri Tabaka la hewa ya Ozoni; Kufanya mafunzo kwa mawakala wa forodha 500 kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa gesi na vifaa vinavyodhibitiwa chini ya Itifaki; Kufanya mafunzo kwa maafisa ugavi na ununuzi 120

kuhusu matakwa ya Itifaki ya Montreal; Kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni; na Kuandaa nyenzo za uelimishaji umma kuhusu hifadhi ya tabaka la ozoni.

## 6) MIRADI MINGINE ITAKAYOTEKELEZWA

### i. Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni kuwezesha shughuli za ujenzi na ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Luthuli I na II Dar es Salaam, na makazi ya Makamu wa Rais Oysterbay Dar es Salaam na Kilimani Dodoma.

### ii. Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za masuala ya Muungano, kuhifadhi kumbukumbu, na kuongeza uelewa  kuhusu Muungano wa Tanzania kwa jamii hususan vijana. Kwa kipindi cha mwaka 2026/27 Ofisi imepanga kuanza shughuli za awali za utekelezaji wa mradi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar.

## 7) BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27 Baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuendelea kuratibu, kusimamia na kushauri utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati ya mazingira kwa lengo la kudhibiti athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; Kuratibu mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inajumuisha masuala ya mazingira kabla ya kuanza utekelezaji; Kusajili na kusimamia utendaji wa wataalamu elekezi wa mazingira; Kutoa elimu na kuhamasisha jamii na wadau kuhusu umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kuzingatia miongozo ya usimamizi wa mazingira kwa maendeleo endelevu na Kufanya tafiti mbalimbali za mazingira ili kuongeza uelewa wa mifumo ikolojia na kuhifadhi bioanuai.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kufanya tathmini katika mifumo ikolojia ya milima, maeneo oevu, vyanzo vya maji, bahari na pwani, mmomonyoko wa fukwe, hali halisi ya bioanuai, ili kubaini hali ya mazingira, kutambua changamoto zilizopo, na kusaidia uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali asilia; Kutoa elimu kwa jamii, wadau na wawekezaji kuhusu umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa maendeleo endelevu; Kudhibiti vyanzo vikuu vya uchafuzi wa mazingira; Kuimarisha usimamizi wa taka hatarishi; Kutekeleza mkakati madhubuti wa kudhibiti kelele na mitetemo inayozidi viwango vilivyowekwa kisheria; Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034); na kuimarisha uwezo wa kitaasisi kwa kuboresha mazingira ya kazi, ikiwemo kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu Njedengwa na Ofisi za Kanda.

## 8) KITUO CHA TAIFA CHA KURATIBU KABONI

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni kitaendelea kutekeleza shughuli

mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha uratibu wa biashara ya kaboni nchini pamoja na uanzishaji wa kituo kama ifuatavyo:- Kuanzisha na kusimamia rejesta ya kidigitali ili kuongeza ufanisi wa usajili na ufuatiliaji wa miradi ya Kaboni; Kwenda kujifunza uendeshaji wa rejesta za kidigitali za miradi ya Kaboni kwenye Nchi zinazofanya vizuri; na Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Biashara ya Kaboni kupitia Mikutano, Warsha, Semina na Mafunzo kwa Makundi Maalum, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kuongeza wigo wa usajili wa miradi ya kaboni ili kulinda mazingira na kuongeza kipato kwa jamii na Serikali; Kuratibu ukamilishaji wa miradi iliyosajiliwa ili iweze kufikia malengo yaliyokusudiwa; Kukamilisha mfumo wa Kidigitali wa Upimaji, Utoaji wa Taarifa na Uthibitishaji (Measurement, Reporting and Verfication – MRV) ili kurahisisha na kuweka uwazi katika uendeshaji wa biashara ya kaboni; na Kuimarisha uratibu wa biashara ya kaboni kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine ni pamoja na Kufanya tafiti na kutoa ushauri kuhusu uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa biashara ya kaboni; Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi mbalimbali ya biashara ya kaboni inayoendelea na kutoa ushauri wa kitaalamu; Kusimamia utekelezaji wa Sheria, kanuni na miongozo zinazosimamia uendeshaji wa biashara ya kaboni nchini; Kusimamia mgawanyo wa mapato yatokanayo na biashara ya kaboni kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo ya biashara ya Kaboni; Kuhuisha kanuni na miongozo ya biashara ya kaboni ili iweze kuendana na wakati na kuleta tija kwa jamii na taifa kwa ujumla; Kuimarisha usimamizi wa vihatarishi, utawala na udhibiti wa ndani ili kuhakikisha malengo ya taasisi yanafikiwa; Kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kupitia ubunifu mbalimbali katika biashara ya Kaboni Nchini ikiwemo kuanzisha hisa za kijani na buluu kupitia biashara ya Kaboni; na kuanzisha mchango wa uzalishaji wa kaboni nchini hasa kwenye usafiri wa Maji na Anga kwa vyombo vinavyotoka nje ya Tanzania.

## F. HITIMISHO NA SHUKRANI

**192.** ***Mheshimiwa Spika***, Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/26 yamechangiwa na ushirikiano mzuri kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Sekta binafsi, Taasisi za Fedha nchini, Asasi Zisizo za Kiserikali za ndani na nje ya nchi; na Wadau mbalimbali.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee ninaomba kutoa shukrani kwa wadau wafuatao: Serikali za Norway; Sweden; Denmark; Japan, Uingereza; India; Korea Kusini; na Ufalme wa Saudi Arabia, Oman, na Qatar. Wengine ni pamoja na: Umoja wa Ulaya (EU); Benki ya Dunia (WB); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF); Mfuko wa Kimataifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (AF); Mfuko wa Kusaidia Nchi zinazoendelea kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (LDCF); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola (FCDO); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO); Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Shirika la Maendeleo la Umoja wa

Mataifa (UNDP); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma za Miradi (UNOPS); Shirika la Chakula Duniani (WFP); na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO).

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** wadau wengine ni pamoja na: Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo - IFAD; Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Mitaji ya Maendeleo (UNCDF); Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF); Mfuko wa Utekelezaji wa Mkataba wa Montreal; Mfuko wa Dunia wa Bioanuai (GBFF); The Good Neighbours Global Impact Foundation; Korea Investment Securities; Kamisheni ya Umoja wa Afrika; Sekretarieti za Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na mazingira na mabadiliko ya tabianchi; Wadau wengine ni pamoja na: TNC, TRC, CRDB, NBC, NMB, Azam Marine, TBC, TADB, ZFF, TFF, UpEnergy Tanzania, BRAC Maendeleo Tanzania, Save the Children na CORUS International.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo na Wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu

wa Rais katika kuimarisha Muungano, hifadhi na usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi na Uchumi wa Buluu kwa maendeleo endelevu.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baada ya shukrani hizo kwa washirika wa maendeleo, ninaomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru **Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa (Mb.),** Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kumshukuru **Dkt. Richard Stanslaus Muyungi,** Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Ndugu **Abdallah Hassan Mitawi,** Naibu Katibu Mkuu (Muungano), **Balozi Baraka Haran Luvanda,** Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), **Mhandisi Mwanasha Rajabu Tumbo,** Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), **Dkt. Albina Andrew Chuwa,** Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC), **Dkt. Immaculate Sware Semesi,** Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) **na Bi.**

**Kathryn Kigaraba,** Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni Nchini (NCMC)**,** Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, NEMC na NCMC kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

**198.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa heshima kubwa na ya kipekee ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kikwajuni, Zanzibar kwa kunipa heshima ya kuwawakilisha tena hapa Bungeni kwa kipindi cha nne mfululizo. Aidha, ninakishukuru sana Chama Cha Mapinduzi kwa kunipa heshima ya kugombea tena katika Jimbo la Kikwajuni, Zanzibar. Ninawaahidi wananchi wa Kikwajuni na Chama Cha Mapinduzi utumishi wenye ari, bidii, weledi, heshima na utiifu.

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwisho lakini sio kwa umuhimu napenda kuishukuru familia yangu pendwa nikianza na Mke Wangu Kipenzi Thania Ali Abdulla na watoto wetu, Riziki Hamad Masauni, Asha Hamad Masauni, Bareek Hamad Masauni na Basit Hamad Masauni kwa upendo wao unaonipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu vyema.

## G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27

**200.** ***Mheshimiwa* Spika,** ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 23,297,959,000.00** kwa ajili ya matumizi ya Fungu 26 (Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,297,959,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 22,000,000,000.00** ni Matumizi Mengineyo.

**201.** ***Mheshimiwa Spika*,** aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 76,686,837,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Fungu 31. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 38,371,992,000.00** ni Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 4,875,325,000.00** ni Mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, **Shilingi 7,096,050,000.00** ni ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na **Shilingi 26,400,617,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 38,314,845,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 14,402,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 23,912,845,000.00** ni fedha za nje.

## H. HITIMISHO

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni www.vpo.go.tz.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.



2026

ofisi ya makamu wa rais